SportPesa
TZS. 861,636,800
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SABAYA** akana kutakatisha milioni 90/-




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Januari 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580833

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Mchepuko adaiwa kuua mke wa mtu

**AMTUHUMU** kutoa ujauzito wake, anaswa na polisi akiwa amejificha jirani na nyumbani...*Endelea ukurasa 2*



Moja kati ya nyumba 27 zilizoezuliwa na mvua iliyoambatana na upepo mkali huku watu wawili wakijeruhiwa katika kijiji cha Banawanu, Kata ya Udonja, wilayani Wanging'ombe, mkoa wa Njombe juzi. **PICHA: ELIZABETH JOHN**

## Mvua yabomoa nyumba 260 Njombe, Morogoro

UKURASA 2

## Sababu za wanafunzi kufeli somo la Hisabati zabainishwa

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akitoa heshima za mwisho kwenye mwili wa kaka yake, Askofu mstaafu wa Kanisa la Anglikana, marehemu Gerald Mpango, wakati wa ibada ya kuaga mwili wake katika kanisa la Anglikana la Mtakatifu Albano, jijini Dar es Salaam jana. **Habari Uk. 04. PICHA: OMR**

**MICHEZO** **SIMBA KUISHANGAZA MTIBWA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa (wa tatu kushoto), akikagua ujenzi wa daraja la Kitengule ambalo linaunganisha Wilaya ya Misenyi na Karagwe, mkoani Kagera jana, baada ya kutembelea kiwanda cha Kagera Sugar Ltd kilichopo mkoani humo. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kagera Sugar Ltd, Seif Ali Seif. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Mchepuko adaiwa kuua mke wa mtu

**Na Woinde Shizza, ARUSHA**

Mwili wa Teddy Malya (31) mkazi wa Ilboru Kisiwani, Arumeru mkoani hapa, umekutwa umetupwa kwenye shamba la migomba huku ukiwa mtupu na baadhi ya majeraha mwilini akidaiwa kuuawa na hawara wake (mchepuko).

Mwili huo ulikutwa eneo hilo jana majira ya saa 2:30 asubuhi na wapiti njia na kuuchukua kwenda kuhifadhiwa katika eneo la kutunzia maiti ndani ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha ya Mount Meru.

Mwanamke huyo anadaiwa kutoonekana siku moja kabla ya mwili huo kugundulika na wapitanjia ukiwa kwenye shamba hilo huku majani yakiwa yamevurugika .

Taarifa za wakazi wa eneo hilo, zimedai kwamba marehemu alikuwa na uhusiano wa siri na mwanamume nje ya ndoa ambaye anadaiwa kutekeleza mauaji hayo. Inadaiwa kuwa mwanamume huyo alikuwa na ugomvi akimtuhumu mwanamke huyo kutoa ujauzito wake, jambo ambalo mume wa marehemu alikanusha.

Mme wa marehemu, Richard Lanyuni (42) alisema aligundua mke wake kuuawa baada ya kupokea taarifa za wapitanjia kuwa kuna mtu amelala kwenye shamba la migomba ndipo alipofika na kukuta ni mkewe akiwa amepoteza maisha.

Akihojiwa na waandishi wa habari, Lanyuni alisema mkewe ambaye hufanya biashara ya kuuza pombe za kienyeji aina ya mbege, hakuonekana kurejea nyumbani muda wa kawaida na ilipotimu majira ya saa saba usiku, aliamua kulala ndipo kesho yake alipata taarifa za kuuawa.

"Mke wangu anafanya biashara ya kuuza pombe za kienyeji siku hiyo hakurejea nyumbani lakini nimeambiwa siku ya tukio alionekana akiwa na kijana mmoja anayefahamika.kwa jina moja la Baraka," alisema Lanyuni.

"Kuhusu mke wangu kuwa na uhusiano na mwanamume huyo, siwezi kujua ila hakuwa na ujauzito. Naomba vipimo vya kitaalamu vifanyike kujua kama kweli alikuwa na ujauzito maana ana shughuli zake mimi siwezi kumchunguza sana," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justin Masejo, alisema Jeshi la Polisi linamshikilia mtu mmoja (jina limehidhadiwa kwa ajili ya uchunguzi) mwenye jinsia ya kiume kwa tuhuma za kumuua mwanamke huyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Mtaa wa Ilkiroriki, Emmanuel Lazaro, mtuhumiwa alikuwa anadaiwa kuwa na uhusiano wa kimapenzi na marehemu enzi za uhai wake.

Mwenyekiti huyo alisema Mallya alikamatwa kutokana na baadhi ya nguo zake na viatu kukutwa eneo la tukio, jambo ambalo waliamini anahusika na mauaji hayo.

"Huyo jamaa alikamatwa kwenye nyumba mojawapo hapo mtaani amejificha na kilichosababisha ni baada ya viatu vyake pamoja na nguo kukutwa eneo la tukio," alisema Lazaro.

Alisema jambo lingine lililowatia wasiwasi ni baada ya kumkuta mtuhumiwa akiwa na majeraha ya meno sehemu mbalimbali za mwili wake, kitendo kinachoashiria walikuwa na purukushani na marehemu kabla ya mauti kumfika.

Lazaro alisema mallya kabla ya mauti kumfika, alionekana akiwa na mtuhumiwa katika baa mojawapo mtaani wakinywa pombe kabla ya kupatikana akiwa ameshafariki dunia.

"Tukio hili limetushtua sana sisi Kama wakazi wa huu mtaa Kka kuwa si la kawaida lakini tumeukuta mwili wa marehemu ukiwa hauna nguo na inaonekana alibakwa kabla ya kuuwawa," alisema Lazaro.

Baadhi ya majira wanadai kwamba mtuhumiwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na marehemu wakidai kwamba mtuhumiwa alikasirishwa na hatua ya marehemu kudai kutoa ujauzito wake jambo ambalo liliibua sintofahamu.

# Mvua yaharibu nyumba 260 Njombe, Morogoro

**Na Waandishi Wetu**

MVUA kubwa iliyoambatana na upepo imesababisha maafa katika vijiji viwili kwenye mikoa ya Njombe na Morogoro kwa kuezua takriban nyumba 260 na kujeruhi watu wawili.

Katika kijiji cha Banawanu mkoani Njombe, nyumba 27 zimeezuliwa na watu wawili kujeruhiwa huku mkoani Morogoro, nyumba 230 zimeezuliwa katika kijiji cha Kisegese, Halmashauri ya Mlimba.

Akizungumza katika Kamati ya Tathimini ya Maafa ya Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Mwenyekiti wa Kijiji cha Banawanu, Watson Mwenda, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 10:00 jioni. Mwenda aliwataja majeruhi kuwa ni Amos Kuyava (45) na Faraja Site (2).

Alisema mvua hizo pia zimeleta maafa katika Kitongoji cha Talibato na kwamba katika vitongoji vingine baadhi ya nyumba zimedondoka.

"Kijiji chetu kina vitongoji vitano lakini kilichoathirika sana ni Kitongoji cha Talibato nyumba 21, Mji Mwema nyumba tatu, Banawanu Kati kumeezuliwa nyumba mbili, Nyaubaga nyumba moja kwa hiyo kwa jumla nyumba zote zilizoezuliwa ni 27,"alisema Mwenda.

"Mvua hizo zimeleta athari pia kwa kujeruhi watu wawili mmoja ni mtu mzima ambaye ameumia na mwingine ni mtoto ambaye amepelekwa Hospitali ya Ikelu lakini anaendelea na matibabu. Hakuna aliyefariki dunia ila watu nyumba zao nyingi zimeezuliwa mapaa na zingine zimebomoka kabisa," aliongeza.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya waathirika wa tukio hilo akiwamo Beatrice Mtivike, waliiomba serikali kuwasaidia chakula na sehemu ya kulala.

"Mimi sina pa kulala nalala jikoni ambako hakuna mlango, nilikua nimeweka mahindi yangu lakini yote yamekwenda na maji pamoja na nguo kwa kweli naomba serikali itusaidie ione namna ya kutusaidia kwa sababu hili janga limetukuta katika kipindi kigumu," alisema Mtivike.

Hata hivyo, alimshukuru Mungu kwa kunusurika katika tukio hilo kwa sababu wakati linatokea alikuwa shambani.

Mwathirika mwingine, Abel Kidegelime, alisema kuezuliwa kwa nyumba yake kumemwathiri kutokana na kupoteza chakula na baadhi ya vifaa kuharibika.

Geofrey Benela alisema tukio hilo limewakuta kipindi ambacho ni cha maandalizi ya kuwapeleka watoto shuleni.

"Janga hili limetukuta kipindi ambacho tunatakiwa kuwapeleka watoto shule, limetudhoofisha sana kimaisha, upepo ulikua mkali ndiyo maana imeleta madhara makubwa," alisema Benela.

Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Wanging'ombe, Frank Ngogo, alitoa pole kwa kaya zilizokutwa na maafa hayo na kuwataka kuwa watulivu katika kipindi hiki.

**MAAFA MLIMBA**

MVUA iliyoambatana na upepo mkali imeezua nyumba zaidi ya 230 katika kijiji cha Kisegese, Halmashauri ya Mlimba, Kilombero mkoani Morogoro na kuwaacha baadhi ya wakazi bila mahali pa kuishi.

Baadhi ya waathirika, wakiwamo Zainab Mpendi na Victor Komba, walikiri kuwa hali zao ni mbaya kutokana na maafa hayo, ambayo yamewafanya baadhi ya wananchi kulala nje na wengine kuhifadhiwa na majirani.

Walisema upepo mkali uliibuka wakati mawingu yalipokuwa yakijipanga kunyesha mvua na kusababisha baadhi ya nyumba kuezuliwa mapaa.

"Hali ilikuwa mbaya. Nilikuwa natokea shambani kwangu manyunyu ya mvua yakiendelea kunisindikiza. Nilipokaribia kijijini, ghafla ulianza upepo mkali ambao ulisababisha tawi la mti karibu yangu kukatika. Nilipofika nyumbani nikakutana na majanga mengine ya nyumba kuezuliwa paa," alisema Mpendi.

Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi, jana alifika kijijini hapo na kushuhudia mazingira ya nyumba zilizoezuliwa na kuwasaidia wananchi waliokuwa katika hali mbaya zaidi Sh. milioni mbili na kuahidi kujenga nyumba ya moja ya wananchi ambaye ni mgonjwa.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kisegese, Manfred Meyambe, alisema hatua walizozichukua baada ya athari hizo ni pamoja na kuhakikisha wanahifadhi wanakijiji waliokuwa na hali mbaya ya kimakazi na kuandaa maeneo ya wazi kwa ajili ya hifadhi.

"Tumefuatilia zaidi ya nyumba 230 zilizopata athari za upepo na tunashukuru kupata msaada kutoka serikalini na kwa mbunge wetu Godwin Kunambi. Mpaka sasa hakuna jambo lililokwama japo bado wananchi wanahitaji msaada zaidi wa kibinadamu," alisema.

**• Imeandikwa na Elizabeth John, NJOMBE na Iddah Mushi, MLIMBA.**

## HABARI KITAIFA

# Sabaya akana kutakatisha fedha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amedai kuwa hakuwahi kutakatisha Sh. milioni 90 wala kutoa mgawo wa fedha kwa vijana wanaodaiwa kuwa ni wake.

Sabaya ambaye ni shahidi wa pili na mshtakiwa wa kwanza katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 na wenzake sita, alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Arusha.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Fridolin Bwemelo, Sabaya alidai kwamba hakuwahi kutoa mgawo wa fedha kwa vijana wanaodaiwa kuwa ni wake kwa kuwa hawafahamu kabisa

"Mheshimiwa hakimu mimi sijatakatisha fedha wala kutoa mgawo kwa mtu yeyote ambaye simfahamu na eneo wanalodai kwamba nilifanya mgawo huo siku hiyo, sikuwapo. Nilikuwa Hai, Kilimanjaro," alidai Sabaya.

Pia alikana kutakatisha Sh. milioni 90 na hakukuwa na sababu kwa upande wa mashtaka kupeleka gari lake mahakamani kama kielelezo cha ushahidi kwa kuwa halihusiani na hati ya mashtaka kwa kuwa alilinunua kwa Sh. milioni 60.

"Gari langu VX V8 T222DBY sikulinunua Januari 22, 2021 lakini limeletwa mahakamani kama kielelezo cha ushahidi ilihali halihusiki katika hati ya mashtaka.

"Mheshimiwa hakimu mashtaka ya kugawa fedha kwa kutakatisha dhidi yangu si ya kweli. Hati ya mashtaka ni batili kwa kuwa hapa mahakamani sina shtaka la kutakatisha fedha nikiwa Dar es Salaam au hoteli ya Tulia Lodge, hivyo shtaka hili ni la uongo kwa kuwa wameshindwa kuthibitisha," alidai.

Sabaya pia alikana kumtuma Mwahomange anayedaiwa kuwa alimwagiza kupeleka pampu kutengenezwa katika Karakana ya mfanyabiashara Francis Mroso.

"Shahidi wa nne wa mashtaka Philemon Kazibira, ambaye ni karani wa Mroso, alidai kwamba aliniona mimi nikiwa nimeambatana na vijana wanne na baada ya hapo niliagiza mfanyabiashara huyo kuitwa kufika ofisini hapo.

"Invoice na ripori, inayodaiwa na shahidi wa nne baada ya pampu kutengenezwa havijawahi kuletwa hapa mahakamani kama uthibitisho kama kuna pampu ilikwenda kutengezwa katika Karakana hiyo. Hakuna kitu kinachothibitisha kwamba pampu ilipelekwa katika eneo hilo," alidai Sabaya.

Akiongozwa na wakili mwingine wa utetezi, Sylvester Kahunduka, Sabaya alidai kwamba maofisa wa TAKUKURU, hawakufuata sheria na pia hawakuwa na kibali cha kusachi.

Sabaya alidai kuna vitu ambavyo vimekamatwa na maofisa wa TAKUKURU na polisi lakini wameficha taarifa zake, hawataki kuziweka wazi.

# Sababu wanafunzi kufeli Hisabati zatajwa

**Na Frank Monyo**

KAMISHNA wa Elimu, Dk. Lyabwene Mutahabwa, ametaja sababu za wanafunzi kufanya vibaya somo la Hisabati katika mitihani ya taifa ikiwamo mazingira ya ufundishaji kutokuwa rafiki na wezeshi.

Sababu nyingine, amesema ni kutokuwapo kwa upendo kati ya mwanafunzi na mwalimu wa somo hilo, hali inayoweka uwoga wa kulielewa somo hilo.

Alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa miongozo minne ya kufundishia elimu ya stadi za maisha kwa kuzingatia afya ya uzazi, Virusi vya Ukimwi (VVU), jinsia na kuhusiana kwa heshima kwa walimu wa shule za msingi na sekondari, iliyoandaliwa na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

"Mlisikia juzi matokeo ya kidato cha nne katika somo la Hisabati yalikuwa si mazuri. Nimefuatilia katika baadhi ya shule nimekuta hivi, mwalimu akitoa hesabu 10 anakuwa na mzigo wa fimbo, mwanafunzi atakayekosa hesabu tano atachapwa viboko vitano, akikosa hesabu tatu atachapwa fimbo tatu. Yaani unapigwa fimbo kulingana na idadi ya hesabu ulizokosa," alisema. Dk. Mutahabwa alisema endapo kuna mwalimu mwenye dhana kwamba anapofundisha akitumia fimbo inasaidia kumjaza akili mwanafunzi, atakuwa anajidanganya na kwamba ualimu hauko hivyo. Aliwashauri walimu wanaofundisha somo la Hisabati kuwa na ushirikiano, upendo na kuwa tayari wakati wote kuwasaidia wanafunzi. Alisema kwa kufanya hivyo, wanafunzi wengi watafaulu somo hilo.


A PRODUCT OF The Coca-Cola Company

KILIMANJARO DRINKING WATER

TAARIFA KWA UMMA

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz

+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422



EAGLE RECOVERIES LIMITED

NOTISI/MNADA

Kwa amri ya Mahakama ya Mwanzo, Buguruni, Dar Es Salaam, tutauza kwa mnada wa hadhara nyumba ya kuishi iliyopo Kidugalo-Chanika, Dar es salaam kufuatia Shauri la Madai/Fedha Na. 25/2021.

MDAI ……………………..OMARI BAKARI LOTA

DHIDI YA

MDAIWA……………………EMANUEL SAHANI

| NA. | JINA LA MDAIWA | SIFA YA DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 01 | EMANUEL SAHANI | NYUMBA KUBWA NZURI YENYE VYUMBA VITATU VYA KULALA, NA INA NYUMBA NDOGO PEMBENI YA VYUMBA VIWILI. | JUMATANO 09.02.2022 KUANZIA SAA 5 ASUBUHI |

MASHARTI YA MNADA:

A). UKAGUZI UNARUHUSIWA KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

B). MALIPO NI 25% YA BEI ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA NA SALIO 75% ITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NNE (14) TU.

C). ENDAPO MNUNUZI ATASHINDWA KULIPA KWA MUDA ULIOTOLEWA, ATAKUWA AMEPOTEZA HAKI ZAKE ZOTE NA NYUMBA/ KIWANJA ITAUZWA TENA

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NA.0683 152 822/0753 351 588 0716 401 534 /0743448888.



NIC Life House 4th Floor, Wing C
Sokoine Drive/Ohio Street,P. O. Box 6100,Dar es Salaam
Tel:+255 22 2112045,Fax: +255 22 2112045

Dev Recoveries Ltd

MARUDIO YA MNADA

NOTISI YA KULIPA DENI NA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **DEV RECOVERIES LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **EQUITY BANK TANZANIA LIMITED,** Tunatangaza marudio ya **MNADA WA HADHARA,** Mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini, mnada utafanyika kuanzia saa 6:00 mchana na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

**MCHANGANUO WA DHAMANA ITAKAYOUZWA .**

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **OCEANIC RESORT/ FLORENCE RWENYEMAMU FRANCIS** | Hati Na. 79320, Kiwanja No.1042-49, Kitalu "B" Mbweni, Dar es Salaam City. Ukubwa wa eneo sqm 10,500. | 25/01/2022 kuanzia saa 06:00 mchana |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, au kama atakavyo kubaliana malipo hayo mteja na Benki
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. Kwa mawasiliano zaidi piga **simu No: 0712390460 / 0788438640**

## HABARI KITAIFA

# Shahidi aeleza washtakiwa kesi ya Mbowe walivyonaswa

**Na Kulwa Mzee**

ASHAHIDI wa 11 wa Jamhuri katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, na wenzake watatu, Koplo Gooluck Minja, ameeleza vielelezo walivyokamatwa navyo mshtakiwa wa kwanza na wa pili ikiwamo bastola, aliyokabidhiwa maeneo ya Rau Madukani, Moshi.

Goodluck alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joachim Tiganga wakati akitoa ushahidi, akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar.

Alidai kuwa Agosti 4, 2020 akiwa kazini kwake Kituo Kikuu cha Polisi Arusha, alipewa maelekezo na Inspekta Mahita Omari kuwa alikuwa anahitajika pamoja na Koplo Francis kwa Mkuu wa Upelelezi wa makosa ya Jinai Mkoa (RCO).

Alidai kuwa walielekezwa kuna kazi wanatakiwa kuifanya, walienda kituoni kuchukua silaha mbili AK 47 wakaenda Moshi kuwasaka watuhumiwa wa kula njama za kufanya vitendo vya kigaidi.

Katika msafara huo, alidai kuwa alikuwa pamoja na ACP Ramadhan Kingai, Inspekta Mahita, Jumanne na Koplo Francis.

"Watuhumiwa walikuwa kwenye grosari, tuliwakamata wawili, Afande Jumanne aliita mashahidi wawili Anita na Esther. Alijitambulisha kwa watuhumiwa, akaamuru mtuhumiwa wa kwanza, Adamu Kasekwa ainuke.

"Afande Jumanne alianza kumpekua kwa kumpapasa kuanzia kichwani alipofika kiunoni akatoa bastola. Kwenye mfuko wa suruali alitoa karatasi ikiwa na dawa zinazodhaniwa za kulevya kete 58,"alidai shahidi.

Alidai kuwa aliendelea kumpekua akakuta simu kwenye mfuko wa suruali, bastola ilikuwa na risasi tatu na magazine, vyote alikabidhiwa. Alidai kuwa Mahita na Kingai waliporejea kwenye gari waliondoka kwenda kituoni na waliambiwa wamtafute mtuhumiwa wa tatu waliyemtaja kwa jina la Kakobe.

Koplo Goodluck alidai walimtafuta mtuhumiwa huyo maeneo mbalimbali kwa maelekezo ya watuhumiwa lakini hawakumpata. Aliyataja maeneo waliyofika kuwa ni Moshi mjini, Aishi Hotel, Bomang'ombe na Sakina, Arusha.

Alidai kuwa Agosti 6, 2020 walifuatilia hadi saa 12 jioni wakaamua kutoka Arusha wakarudi Moshi wakaelekezwa watuhumiwa wanatakiwa kupelekwa Dar es Salaam ndipo walipowasafirisha wakafika Dar es Salaam Agosti 7, 2020 alfajiri katika Kituo Kikuu cha Polisi na kuwakabidhi chumba cha mashtaka.

"Agosti 7 nilikabidhi simu aina ya Itel na Techno, silaha, risasi tatu pamoja na magazine kwa Sajenti Nuru. "Sajent Nuru nilimkabidhi pistol A5340, magazine na risasi tatu. Afande Swila nilimkabidhi simu pamoja na line zake," alidai.

Upande wa utetezi haukuwa na pingamizi, mahakama ilipokea ikawa kielelezo namba 36 cha upande wa Jamhuri.

Shahidi alidai Agosti 8, mwaka huo, waliwahamisha watuhumiwa kutoka Kituo Kikuu cha Polisi na kuwapeleka Kituo cha Mbweni ambako waliwakabidhi katika chumba cha mashtaka na kuondoka.

Baada ya hapo, alidai kuwa waliendelea kuwasaka watuhumiwa wengine na Agosti 9, 2020 walikamata mshtakiwa Halfani Bwire na kumpeleka Kituo cha Polisi Chang'ombe na simu aliyokutwa nayo alikabidhiwa pia.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Halfani Bwire, Kasekwa na Ling'wenya ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwemo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi.

# Dk. Mpango amlilia kaka yake, asema alikuwa nguzo muhimu

**Na Mary Geofrey**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amemlilia kaka yake, Askofu Mstaafu Dk. Gerald Mpango, huku akimwelezea kuwa alikuwa nguzo yake kuu katika elimu kutokana na kumhimiza kusoma kwa bidii, jambo analojivunia hata sasa.

Dk. Mpango aliyaeleza hayo katika ibada ya kuuaga mwili wa Askofu Mstaafu Mpango jana katika Kanisa Kuu la Anglikana la Mtakatifu Albano, Dayosisi ya Dar es Salaam.

Alisema kaka yake alikuwa akimhimiza kusoma, hivyo aliwataka wazazi nao kuwahimiza watoto wao kusoma kwa bidii. Pia alisema kaka yake huyo alikuwa kama baba kwake na alikuwa na busara za kuwashauri wadogo na wakubwa.

Aidha, Dk. Mpango alitumia fursa hiyo kumuombea msamaha kaka yake kwa ndugu, jamaa na mafiki ambao aliwahi kuwakosea.

Dk. Mpango pia alitoa shukrani zake za dhati kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa msaada aliowapatia kutokana na kumpoteza kaka yake, viongozi wa serikali, viongozi wa dini, chama , ndugu jamaa na marafiki.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, akitoa salamu za rambirambi katika ibada hiyo alisema: Matatizo na furaha ni sehemu ya maisha. Niwatie moyo kuwa hili nalo litapita na binadamu tujiandae kwa nyakati za kulia na furaha."

Naye Mwenyekiti wa CCM mkoa wa Dar es Salaam, Kate Kamba, alishukuru kwa utumishi wa Askofu Mstaafu Mpango na kuwapa pole familia yote na mjane. Msajili wa Kanisa la Anglikana Tanzania, George Mandepo, alisema wanatambua mchango wa Askofu Mstaafu Dk. Mpango kwa kazi kubwa aliyoifanya enzi za uhai wake na kuandika kitabu.

Naye Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Alex Malasusa, alisema Askofu Mstaafu Mpango alikuwa akihubiri katika makanisa ya KKKT na alikuwa akisimamia neno na alikuwa akitoa ushauri na kuzungumza nao mara kwa mara.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA**
**TASAC**

**TANZIA**

MKURUGENZI MKUU WA SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC), KWA MASIKITIKO MAKUBWA ANATANGAZA KIFO CHA MSAJILI WA MELI NA MKURUGENZI WA IDARA YA ULINZI NA USALAMA WA VYOMBO VYA USAFIRI MAJINI NA UTUNZAJI WA MAZINGIRA YA BAHARI (DMSE) **MHA. ALFRED WARYANA MISSANA** KILICHOTOKEA TAREHE 20 JANUARI, 2022 KATIKA HOSPITALI YA RABININSIA, TEGETA, DAR ES SALAAM.

MKURUGENZI MKUU ANATOA SALAM ZA POLE KWA FAMILIA, WAFANYAKAZI NA WOTE WALIOGUSWA NA MSIBA HUU.

HAKIKA ATAKUMBUKWA KWA **"UCHAPAKAZI, UADILIFU NA UZALENDO KATIKA KIPINDI CHAKE CHOTE CHA UHAI WAKE".**

TUNAWAOMBEA WOTE FARAJA MLIOGUSWA NA MSIBA HUU KATIKA KIPINDI HIKI KIGUMU CHA MAJONZI. MUNGU AILAZE ROHO YA MAREHEMU MAHALI PEMA PEPONI.
AMEN

Imetolewa na;

**MKURUGENZI MKUU**
**SHIRIKA LA UWAKALA WA MELI TANZANIA (TASAC).**



*MHA. ALFRED WARYANA MISSANA*

**Jengo la PPF Tower, Sakafu ya 8, Kiwanja Na. 20/21, Mtaa wa Garden/Ohio,**
**S. L. P. 989, Dar es Salaam - Tanzania, Simu: +255 222 127 314, Nukushi: +255 222 127 313,**
**Barua Pepe: dg@tasac.go.tz, info@tasac.go.tz, Tovuti: www.tasac.go.tz**

TANGAZO

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU
# WAJIBU WA KUDAI RISITI ZA EFD KWA WANUNUZI WA BIDHAA AU HUDUMA

**Dar es Salaam, Januari 21, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wanunuzi wote wa bidhaa au huduma kuhakikisha wanadai risiti za EFD pale wanapofanya manunuzi ili kutimiza wajibu wao wa kisheria. Aidha, wanunuzi wote wa bidhaa au huduma wanakumbushwa kuhakikisha thamani iliyo kwenye risiti ni sawa na kiasi cha fedha walicholipa au wanachotakiwa kulipa.

**Kifungu cha 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438** kinatoa wajibu kwa muuzaji wa bidhaa au huduma kutoa risiti ya EFD pindi anapofanya mauzo na vilevile **Kanuni ya 55(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya Mwaka, 2016** inampa wajibu mnunuzi wa bidhaa au huduma kudai risiti pale anapofanya manunuzi na kuionyesha kwa Kamishna au Afisa wa Kodi pindi anapotakiwa kufanya hivyo.

Ni kosa kisheria kwa mnunuzi yeyote kutokudai risiti pindi anaponunua huduma au bidhaa. Kwa mujibu wa **Kifungu cha 86(4) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438**, mnunuzi atakayebainika kutodai risiti atawajibika kulipa faini isiyopungua **TZS 30,000** na isiyozidi **TZS 1,500,000** kama adhabu.

Hivyo wanunuzi wote wa bidhaa au huduma wanakumbushwa kuendelea kudai risiti za EFD na iwapo muuzaji wa huduma hiyo au bidhaa hatampatia risiti, mnunuzi anatakiwa kutoa taarifa katika Ofisi za TRA zilizopo jirani naye kama inavyoelekezwa kupitia **Kanuni ya 55(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya Mwaka, 2016** au kupiga simu kupitia namba ya bure ya huduma na elimu kwa mlipakodi ambazo ni **0800 750 075 au 0800 780 078**.

Kuanzia tarehe **01/02/2022** TRA itafanya operesheni maalumu za ukaguzi wa risiti za manunuzi ya bidhaa na huduma katika maeneo mbalimbali nchi nzima ikilenga kuhakikisha kila mnunuzi anatimiza wajibu wake wa kisheria kwa kudai risiti pale anapofanya manunuzi.

***Epuka usumbufu, ukiuza toa risiti na ukinunua dai risti.***

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;

**A.J Kidata**
**KAMISHNA MKUU**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

216662702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mungu ibariki Tanzanite ikinusa Kombe la Dunia

**WAKATI** vigogo wa soka wakiendelea kupambana huko Cameroon kuwania taji la Afrika (AFCON 2022), Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake ya umri chini ya miaka 20 (Tanzanite Queens), inatarajia kushuka dimbani kuvaana na wenzao kutoka Ethiopia kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia.

Mechi hiyo ya Tanzanite Queens inayoongozwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime dhidi ya Ethiopia itachezwa kesho kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Tanzanite Queens ilifika hatua hiyo baada ya kuwaondoa Eritrea na baadaye Burundi ambapo katika mechi ya marudiano ilicheza ugenini Bujumbura ikiwa na wachezaji nane uwanjani kutokana na nyota wengine kukutwa na changamoto ya ugonjwa wa Uviko 19.

Wawakilishi hao wa Tanzania wamebakiza mechi tatu ili kupata tiketi hiyo ya kushiriki fainali hizo za Dunia, ambapo itakuwa ni kwa mara ya kwanza. Fainali hizo zitafanyika baadaye mwaka huu nchini Costa Rica.

Huu ni wakati mwingine muhimu kwa serikali, makampuni, taasisi na wadau mbalimbali wa michezo kuisapoti timu hiyo ili itimize malengo yake ya kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo ya kimataifa.

Tanzanite Queens inakabiliwa na dakika 90 za nyumbani na nyingine kama hizo itakapokwenda Ethiopia. Ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele, wadau wanatakiwa kukaa karibu na wachezaji wa timu hiyo kwa kuwapa motisha mbalimbali ambazo zitawaongezea nguvu ya kupambana kwenye michezo hiyo inayowakabili.

Tunaamini kwa upande wa ufundi, makocha wamefanya kazi yao ipasavyo na sasa wadau nao wanatakiwa kuwakumbuka 'mabinti' hawa ambao wanapambana kuhakikisha nchi inaweka historia kwa kupata tiketi ya kushiriki fainali hizo za dunia.

Ni ukweli unaofahamika timu hiyo haina udhamini hivyo, maandalizi yake yanakumbwa na changamoto mbalimbali kwa sababu Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), linahudumia pia timu nyingine za taifa huku pia ikiendesha mafunzo mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya mchezo huo unaopendwa zaidi.

Tunayakumbusha makampuni na taasisi mbalimbali kuacha kusubiri mpaka pale Tanzanite Queens inapokwenda katika fainali za dunia na kuanza kuwapatia zawadi, muda sahihi wa kuishika mkono timu hiyo ni sasa wakati ikiendelea na maandalizi.

Inafahamika wachezaji hao wanahitaji vifaa vya michezo, mlo kamili, malazi bora lakini pia posho kwa ajili ya kujikimu mahitaji binafsi, jitokezeni kuwashika 'mkono' mabinti hawa ambao wamebakisha mechi chache kuweka rekodi ambayo Tanzania haijawahi kufikiwa.

Lakini tunawakumbusha wachezaji pamoja na changamoto wanazokutana nazo, wanatakiwa kuendelea kujituma kwa sababu mashindano haya ni daraja la kutangaza vipaji vyao.

Mawakala na makocha kutoka sehemu mbalimbali wamekuwa wakizifuatilia mechi zinazochezwa na mataifa yaliyobakia kwenye michuano hii ili kusaka nyota wa kuwasajili kwenye klabu zao. Hivyo wachezaji wasikatishwe tamaa na badala yake watumie michuano hii kujitangaza wakitarajia kuzivutia klabu nyingine za nje ya Tanzania au mataifa ya Ulaya.

Tunaamini mpira wa miguu umesaidia kuwapa ajira wachezaji hawa wanawake kama ilivyo kwa kaka zao, lakini ikumbukwe bila mzazi au mlezi kumpa nafasi au kuthamini kipaji cha binti huyu, mafanikio ya mchezaji huyo yatakuwa na milima na mabonde. Umefika wakati jamii ikabadilika kwa kuendelea kuwapa ushirikiano wachezaji wanawake ili kufikia ndoto zao. Kwenye umoja na ushirikiano, hakuna ambaye atashindwa kufikia malengo yake.

Safari ya kuelekea nchini Costa Rica inawezekana, Mungu ibariki Tanzanite Queens, Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ni hatari sana Simba SC, Yanga kwenda Manungu

Na Adam Fungamwango

**KWA** mara ya kwanza baada ya miaka 23, Mtibwa Sugar inaipokea Simba kwenye Uwanja wake wa Manungu, Turiani,mkoani Morogoro.

Inasadikiwa uwanja huo unaingiza watazamaji 1,000. Hata hivyo, Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru amesema lengo lao leo kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania bara ni kuingiza mashabiki 2,500.

Bodi ya Ligi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imeafiki mechi kati ya Mtibwa Sugar dhidi ya Simba kuchezwa kwenye uwanja huo.

Ni kweli uwanja umekidhi vigezo vyote vya kuchezea Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini nafikiri kwa mazingira na utamaduni wa soka la nchi hii, bado ulikuwa haukidhi vigezo vya kuzipokea timu zenye mashabiki wengi, si wa Simba tu, bali hata Yanga.

Katika mazingira ya nchi yetu na utamaduni wa Simba na Yanga ni timu ambazo zimebahatika kukusanya mashabiki kila kona ya nchi hii, tofauti na nchi za wenzetu Ulaya na hata nchi kadhaa Afrika, ambapo kila jimbo, mkoa eneo una timu zake, na mashabiki wake ni wa eneo husika.

Mfano huwezi kukuta mtu kutoka Kigoma akashabikia timu ya Dar es Salaam, lakini hii ni tofauti na nchi hii ya Tanzania. Huku ni Simba na Yanga.

Kama historia inavyojieleza, Simba haijaenda Manungu kiasi cha miaka 23 iliyopita, hiyo tosha itafanya kuwe na mashabiki wengi sana, hivyo kiusalama haitokuwa vizuri.

Ni kweli tumeambiwa usalama utakuwa mkubwa kwa mashabiki na mali zao, lakini ukweli unabaki pale pale Uwanja wa Manungu ni mdogo, hauwezi kuingia mashabiki watakaotoka Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na vitongoji vyake na hata mikoa jirani kama, Dodoma.

Tunaona mechi ambazo Simba au Yanga inacheza mikoani kwenye viwanja vikubwa kama Sheikh Amri Abeid, CC Mkwakwani, Ushirika, Ali Hassan Mwinyi, Sokoine na vingine vinajaa pomoni na kundi lingine la mashabiki linabakia nje ya uwanja, inakuwaje kwenye uwanja mdogo kama huo?

Hata kama Jeshi la Polisi na walinzi, wakikataza mashabiki wote waliotoka Dar es Salaam, Pwani na Morogoro mjini, na wakawaruhusu mashabiki wa Turiani tu kuingia, bado hautotosha.

Kinachotaka kufanyika hapo ni kuingia kiasi hicho cha watu tu, lakini inavyoonekana kabisa kazi itakayokuwapo ni kuwazuia watu waliokuwa nje kuingia uwanjani. Hiyo itakuwa ndiyo kazi kubwa namba moja ya Jeshi la Polisi na walinzi wengine kwenye mechi ya leo, achilia mbali ya pili ambayo ni kulinda ndani ya uwanja na mengineyo.

Nina uhakika mashabiki wengi kutoka Dar es Salaam, Pwani, vitongoji vya Morogoro na Dodoma watakuwepo uwanjani kila mmoja akitaka kujaribu kuingia kuangalia mechi hiyo, ndipo tatizo litakapoanza.

Mtu ametoka mbali kuja kuitazama Simba, unadhani atakubali kweli kuondoka kirahisi bila kuangalia mechi?

Kwenye mechi hizo pia hukusanya wanawake na watoto ambao nao baadhi watakuwa ndani ya uwanja na wengine nje, kitu ambacho ni hatari kama kuna baadhi watataka kulazimisha kuingia.

Hata kama watadhibitiwa kwa nguvu, lakini tayari kutakuwa na dosari ya baadhi ya watu kuumia.

Tumewahi kushuhudia maafa baada ya watu wakiwamo watoto hapa hapa nchini, kulazimisha kuingia uwanjani, si kwenye soka, bali kwenye masuala mengine ya kijamii, nadhani hatujajifunza kutokana na hilo.

Huko nje ya nchi tumewahi kushuhudia maafa kama hayo, baada ya mashabiki wa soka kulazimisha kutaka kuingia uwanjani.

Sisemi kama mechi itakuwa na vurugu, au lazima itokee leo, la hasha, lakini ukweli unabaki pale pale kuichezesha Simba, au Yanga kwenye uwanja kama wa Manungu ni hatari.

Mtoto akicheza na wembe, hata kama haukumkata, lakini bado kuchezea kwake wembe ni jambo la hatari.

Nitoe wito tu kwa Bodi ya Ligi na TFF, hata baada ya mechi ya leo, iliangalie tena suala hili kwa jicho la tatu.

Hatuzitetei timu hizi ili zisicheze kwenye viwanja vya ugenini, lakini tunaangalia ukweli zinakuwa na mashabiki wengi, ambao pia baadhi yao wanakuwa na mambo mengi, ikiwamo mihemko kwa uwanja kama Manungu ni rahisi sana kuingia hata uwanjani wakati mechi inachezwa, au mara tu baada ya kumalizika.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU MABORESHO YA MFUMO WA UKUSANYAJI KODI UNAOTUMIKA KUTOA RISITI ZA KIELEKTRONIKI

**Dar es Salaam, 20 Januari, 2022**
Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha walipakodi wote wanaotumia mashine za kutolea risiti za kielekitroniki (EFD) kuwa, wanatakiwa kufanya maboresho ya mashine zao ili kuendana na matakwa ya mfumo wa kutoa risiti za kielekitroniki zenye **"QR Code"** zinazohakikiwa moja kwa moja na mfumo.

Hivyo, Mlipakodi anaombwa kufika kwa wakala wa mashine za EFD ili kufanya maboresho kwenye mashine kuendana na itifaki mpya ya mawasiliano ijulikanayo kama Protocol 2.1 inayoendana sambamba na maboresho ya mfumo wa EFDMS ambao uhakiki moja kwa moja risiti na ankara mara zinapotoka kwenye mashine ya kielektroniki ya kutolea risiti.

Ikumbukwe kuwa tarehe **7 Desemba 2020,** Mamlaka ilitoa taarifa kwa Umma kupitia vyombo vya habari, hususani magazeti, kuhusu maboresho haya sambamba na hitaji la kuboresha mashine za EFD ndani ya kipindi cha siku thelathini kuanzia tarehe ya tangazo lile. Mamlaka pia ilitoa nyongeza ya kipindi cha siku 30 kwa walipakodi wenye mashine ya EFD ambao hawakukamilisha maboresho au kununua mashine mpya zinazoendana na maboresho ya mfumo.

Baada ya kipindi kilichotolewa awali kupita, Mamlaka imefanya tathmini na kufuatilia utekelezaji wa agizo hilo na kubaini kuwa bado kumekuwepo na baadhi ya Wafanyabiashara ambao bado hawajatekeleza agizo la kuboresha mashine zao za EFD kuendana na itifaki hiyo mpya ya mawasiliano ya Protocol 2.1.

Kwa tangazo hili, Mamlaka inatoa agizo kuwa tarehe **28 Februari 2022** ndiyo siku ya mwisho kwa wafanyabiashara wote ambao bado hawajafanya maboresho katika mashine zao wafanye hivyo ndani ya kipindi hiki. Baada ya hapo Mamlaka itachukua hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuzifungia mashine zote za EFD ambazo zitakuwa bado hazijafanyiwa maboresho hayo.

***"Pamoja Tunajenga Taifa"***

**Imetolewa na**

**MKURUGENZI WA ELIMU NA HUDUMA KWA MLIPAKODI**

# Tanzania, Zambia zakubaliana utaratibu usafirishaji magari

**Na Thobias Mwanakatwe,**
TUNDUMA

TANZANIA na Zambia zimekubaliana wateja wanaoingiza magari kutoka nje kupitia Bandari ya Dar es Salaam na zingine nchini, watakuwa huru kuchagua magari yao yaendeshwe na dereva wa nchi yoyote kuyapeleka au kuyafikisha anakotaka.

Makubaliano hayo yalifikiwa jana katika kikao cha pamoja kati ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, na Mkuu wa Jimbo la Muchinga nchini Zambia, Henry Sikazwe, kilichofanyika ukumbi wa forodha katika mpaka wa Tunduma.

Kikao hicho kiliwashirikisha viongozi wa vyama vya waendesha magari madogo na makubwa yanayotolewa Tanzania kwenda Zambia, maarufu kama IT kutoka nchi zote mbili.

Kikao hicho cha ujirani mwema kilifanyika kutokana na madereva wa Zambia kutishia kuwapiga madereva wa Tanzania watakaonekana wakiendesha magari ya IT kuyapeleka nchini kwao.

Madereva hao walitaka madereva wa Tanzania wawe wanayachukua magari hayo kutoka bandarini na kuyaendesha hadi Tunduma tu na wao (wa Zambia) wayaendeshe hadi Zambia na hadi katika nchi za Zimbabwe na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika kwa kikao hicho, Mgumba alisema wamekubaliana kuwa mteja mwenye gari ndiye ataamua amtumie dereva wa taifa gani kuendesha gari lake na kulifikisha anakotaka.

Mgumba alisema kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa madereva wa Tanzania ambao wamekuwa wakihoji inakuweje gari akabidhiwe yeye kutoka bandarini lakini anapofika Tunduma anaambiwa amkabidhi dereva wa Zambia.

Alisema utaratibu huo ulikuwa ukisababisha hasara kwa madereva wa Tanzania ambapo gari anapomkabidhi dereva mwingine, pindi linapoharibika au kupata ajali, mwenye gari anakuwa hamjui dereva wa Zambia na badala yake dereva wa Tanzania ndiye anaambiwa alipe hasara hiyo.

Kwa mujibu wa Mgumba, makubaliano hayo yatakuwa na faida pande zote mbili na kwamba utaratibu huo utakuwa ukifanyika katika kipindi cha ndani ya miezi sita kuanzia sasa wakati serikali zote mbili zinatafuta utaratibu mpya wa kudumu utakaokuwa ukitumika.

Jambo lingine walilokubaliana, kwa mujibu wa Mgumba, ni kuandaa kikao kingine cha ujirani mwema ambacho kitakuwa mahususi kwa ajili ya kujadili changamoto za kibiashara zinazozikabili nchi zote mbili ili kuzipatia ufumbuzi kwa lengo la kujenga mazingira mazuri ya kibiashara katika nchi hizo.

Mgumba na Sikazwe waliwahakikishia madereva wa pande zote mbili kuwa serikali za nchi zote zitahakikisha zinaimarisha usalama kwa madereva, hivyo wasiwe na wasiwasi wa kufanya kazi zao.




Ofisa Huduma kwa Wateja Makao Makuu NMB, Suzan Manga (kulia), akizungumza na mmoja wa washindi wa droo ya tatu ya NMB MastaBata Kivyakovyako, iliyochezeshwa jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Ofisa Mwandamizi Idara ya Kadi NMB, Said Kiwanga na Mwakilishi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Elibariki Sengasenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Qatar Airways kuendelea kutoa huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Ndege la Qatar Airways limetangaza kuongeza wigo wa safari za ndege katika nchi mbalimbali duniani, sambamba na kuendelea kutoa huduma bora kwa wasafiri wake.

Taarifa iliyotolewa na shirika hilo, ilieleza kuwa pia linajivunia kutimiza miaka 15 ya kutoa huduma Tanzania tangu liliopoanza rasmi Januari 9, 2007 kwa safari kutoka Dar es Salaam hadi Mji Mkuu wa Qatar, Doha.

Makamu wa Rais wa Qatar Airways Afrika, Hendrik Dupreez, alisema katika taarifa hiyo kuwa wanajivunia kwa miaka hiyo kuitumikia Tanzania na kuunganisha nchi na mtandao wao wa kimataifa.

Alisema maadhimisho ya miaka 15 yanaimarisha zaidi uhusiano wa Qatar na Tanzania na uwezo mkubwa ambao njia ya Dar es Salaam imekuwa na mafanikio sana.

"Tunatarajia miaka mingi zaidi kuwaunganisha wasafiri kutoka sehemu mbalimbali duniani, ili kujionea utamaduni na wanyamapori wa kipekee Tanzania," alisema Dupreez.

Alisema Qatar Airways itaendelea kushirikiana na wafanyabiashara na wasafiri wa burudani kuendelea kuwafikisha sehemu mbalimbali wanazokwenda katika bara la Afrika, Ulaya, Asia na Amerika.

Mbali na usafirishaji abiria, alisema Qatar Airways inasafirisha bidhaa na mizigo kama vile dawa, vifaa vya teknolojia, samaki, nyama na maua kwenda mahali kwenye mtandao, husani katika nchi za Hong Kong, Uholanzi.

Dupreez alisema Qatar Airways kwa sasa inaendelea kujenga upya mtandao wake na kwamba kwa sasa ina zaidi ya vituo 140 duniani vikiwamo Zanzibar na Kilimanjaro.

Katika sehemu ya kusherehekea miaka 15, Qatar Airways ilifanya tafrija katika Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) kwa wafanyakazi wake kugawa zawadi mbalimbali kwa abiria waliokuwa katika ndege QR 1499 na QR 1476.

# TPA yatakiwa kuwekeza katika TEHAMA

**Na Enock Charles**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imetakiwa kuwekeza katika Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) itakayosaidia kufanya kazi kwa ufanisi na kwa muda mfupi.

Uwekezaji huo pia utasaidia kuongeza kiwango cha watumiaji wa bandari hiyo na mapato yatokanayo na tasnia hiyo ya uchukuzi.

Akizungumza alipotembelea Bandari ya Dar es Salaam juzi, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alisema matumizi ya teknolojia yatarahisisha utendaji kazi, hivyo kuvutia wateja wa nje kuitumia bandari tofauti na ilivyo sasa ambapo asilimia kubwa ya mizigo inayoingia ni kwa matumizi ya ndani ya nchi.

"Ni lazima tuwekeze kwenye teknolojia ndiyo maana wenzetu wa China wanaongoza. Ukienda Singapore ni bandari ambayo inafanya vizuri sana duniani, ukienda Shanghai ni bandari ambayo inafanya vizuri sana duniani.

"Hiyo yote ni kwa sababu wamewekeza na kuwekeza kule ni pamoja na mifumo yao ya teknolojia kwa maana ya TEHAMA na mimi nawashauri kwamba suala la TEHAMA halina mbadala," alisema Mwakibete.

Alisema mfumo huo utasaidia kuziona meli miezi kadhaa kabla hazijafika bandarini hapo ili taasisi zote zinazohusika na bandari zikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kujua mapema na kufanya taratibu zao na kupunguza muda utakaotumika pindi meli inapofika nchini.

"Kilichopo sasa hivi ukimuuliza ndugu yangu Eric (Hamissi) hapa (Mkurugenzi Mkuu wa TPA) hajui hata mapato ya siku kwa siku yanayoingizwa na bandari yake maana yake mpaka atumie mfumo wa kuzunguka kawaida," alisema Mwakibete.

Hamissi alisema amepokea maagizo hayo na kuahidi watayafanyia kazi ndani ya kipindi kifupi ili kuweka mifumo inayosomana baina ya taasisi takribani 32 zinazofanya kazi na mamlaka hiyo.

"Changamoto ambayo mheshimiwa Naibu Waziri ametupa leo ambayo pia Mheshimiwa Rais alizungumzia Desemba 4 alipokuja hapa ni kuhusiana na mifumo kwamba tuwe na mifumo itakayosomana maana hapa tuna taasisi zaidi ya 32 ndani ya bandari," alisema Hamissi.

Kuhusu malengo mengine ya mamlaka hiyo ndani ya mwaka wa fedha 2021/22 alisema mojawapo ni kupitisha mizigo ya kiwango cha tani milioni 18 ambapo mpaka Desemba 31, 2021 ilikuwa imeshafikisha tani milioni 9.1 na kuvuka zaidi ya asilimia hamsini ya lengo hilo.

Alisema mamlaka hiyo imejipanga kuhakikisha katika mizigo hiyo inayoingia nchini, mingi iwe ni ya kusafirisha nje ya nchi (transit) ili kuongeza mapato kupitia fedha za kigeni tofauti na ilivyo sasa ambapo asilimia 70 ya mizigo hiyo huishia ndani ya nchi.



## Serikali za mitaa vinara kwa rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI za mitaa, vijiji, kata na halmashauri zimetajwa kuwa na asilimia 36 za malalamiko mengi ya rushwa, zikifuatiwa na sekta ya ardhi ambayo ina asilimia 19.

Wakati sekta hizo mbili zikiongoza kwa madai ya rushwa, elimu inashika nafasi ya tatu kwa kuwa na asilimia 11 na mahakama asilimia tisa.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema jana kuwa afya inalalamikiwa kwa asilimia saba ya matukio ya rushwa ikifuatiwa na fedha yenye asilimia tano.

Kibwengo alisema hayo wakati akitoa taarifa ya robo tatu ya mwaka katika hafla iliyofanyika ofisi za taasisi hiyo jijini Dodoma.

Alisema asilimia hizo si nzuri, hivyo watumishi walioko kwenye maeneo hayo wanapaswa kujitathmini ili kuondokana nayo.

"Serikali za mitaa zinaongoza kwa upande wa ardhi wameshuka ambao kila mara wamekuwa wakiongoza kwa kulalamikiwa kwa vitendo vya rushwa," alisema Kibwengo.

Pia alisema taasisi hiyo imekagua miradi 596 yenye thamani ya Sh. bilioni 20.6 ikiwamo kutoa ushauri ili kukamilishwa kwa wakati.

Kibwengo alisema wakati wa ukaguzi wa miradi hiyo ushauri ulitolewa katika miradi ambayo ilikutwa na changamoto na kuwapa muda wa kuifanyia kazi ili ikamilike wananchi waweze kuitumia.

Pia alisema wamefuatilia miradi minne ambayo ilikataliwa mwaka jana na kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru. Kati ya hiyo, mitatu ilikutwa na dosari ndogo ndogo ambazo zilijadiliwa na kurekebishwa.

"Mradi mmoja kati ya hiyo ulionekana kuna malipo yalifanyika bila kazi husika kutekelezwa, hivyo tunashirikiana na halmashauri husika kufuatilia marekebisho," alisema Kibwengo.

Katika kuzuia vitendo vya rushwa, alisema taasisi imefanya uchambuzi wa mifumo tisa ya utendaji na utoaji huduma katika mkoa wa Dodoma ikiwamo kushiriki semina 11 za kujadili matokeo ya uchambuzi wa mifumo hiyo.

# Bashe awatoa hofu wananchi kuhusu uhakika wa chakula

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Husein Bashe, amesema hakuna Mtanzania atakayekufa kwa sababu ya njaa kwa kuwa serikali ina akiba ya kutosha ya chakula.

Bashe alisema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari huku akisisitiza kuwa Watanzania hawana sababu ya kuogopa mabadiliko ya hali ya hewa yanayochangia kutokuwapo kwa mvua kwa kuwa serikali imejiwekea mikakati ya kutoa chakula kwa jamii na si kuwapa wafanyabiashara.

"Hakuna mtu atakayekufa na njaa. Serikali ina akiba ya chakula cha kutosha, hivyo hakuna sababu ya kuhangaika,"alisema Bashe.

Alisema wanachakula cha kutosha katika maghala, hivyo hakuna haja ya kuingia woga wowote kwa kuwa serikali haitaruhusu wafanyabiashara wauze mahindi kwa bei ya juu.

Kwa mujibu wa Bashe, kuna mifumo mingi ambayo itatumika kuhakikisha wananchi wote wanapata chakula cha kutosha katika mikoa mbalimbali nchini.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka wananchi kutokuwa na wasiwasi juu ya mabadiliko ya hali ya hewa yaliyotangazwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) yanayosababisha mabadiliko ya mvua.

Kuhusu kupanda kwa bei ya mbolea, Bashe alisema hilo si nchini tu bali ni sehemu kubwa duniani kote ndiyo maana imepanda maradufu tofauti na ilivyokuwa awali.

"Bei ya mbolea imepanda duniani kote hivyo kila mmoja anapaswa kulijua hilo. Lakini serikali itahakikisha suala hilo haliwaletei shida wakulima," alisema Bashe.




Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Prof. Faustin Kamuzora (kulia), akiwa amekaa kwenye moja ya madawati 50 yaliyotolewa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB), kwa Shule ya Msingi Kitunga, Wilayani Muleba, mkoani humo mapema wiki hii. Msaada huo ni sehemu ya Sh. milioni 36.3 ambazo benki hiyo imezitumia kukarabati vyumba viwili vya madarasa na kujenga vyoo vya walimu shuleni hapo. Kushoto ni Mkurugenzi wa Biashara na Wateja Wakubwa wa TCB, Adolphina William. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakuu wa mikoa, wilaya wapewa kibarua

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amewaagiza wakuu wa mikoa, wilaya, wakurugenzi wa halamashauri na wakuu wa shule kusimamia kampeni maalumu ya upandaji miti katika maeneo yao.

Jafo alitoa agizo hilo juzi jijini Dodoma alipokuwa akizindua kampeni ya upandaji miti kwa wanafunzi wa shule na vyuo nchini.

Alisema kila mmoja katika nafasi yake akisimamia kampeni hiyo ya upandaji na utunzaji miti, mazingira yatakuwa mazuri na hakutakuwa na mabadiliko ya tabianchi

"Imani yangu kila mmoja atahakikisha jambo hili linakuwa endelevu. Sitapenda kuona tena miti tunayoipanda haitunzwi. Natamani sana nikitembelea miti hii kwa awamu nyingine, nikute inaendelea kukua," alisema Waziri Jafo.

Pia alisema ajenda ya kupanda miti ianze kwa wanafunzi kwa kuwa bado jamii haina uelewa katika suala la utunzaji wa mazingira. Jafo pia aliwashukuru wadau mbalimbali kuamua nchi isonge mbele katika ajenda ya utunzaji wa mazingira kwa kuibeba na kuisimamia katika kila hatua.

Kadhalika, Waziri Jafo aliwataka Watanzania wote kuhakikisha wanasimamia usafi wa mazingira katika maeneo yao kila muda.

"Kila Mtanzania anatakiwa kuonesha mfano katika kampeni hii. Sitatamani kuona tunamwacha mtu yeyote nyuma katika upandaji na utunzaji wa miti," alisisitiza.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, David Silinde, aliagiza shule zote kufufua klabu za mazingira na kutekeleza agizo hilo kwa vitendo kwa kuwa bila kutunza mazingira ni wazi wanafunzi watashindwa kujifunza kwa furaha.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, alisema mkoa wake utahakikisha unazitumia vizuri mvua ambazo zimeanza kunyesha kupanda miti.

"Wakati vijijini hivi sasa tunawahamasisha kuanza kulima, sisi wa mjini tunahamasishana kuanza kupanda miti ili angalau kila kaya kuwa na mti mmoja wa kivuli na miwili ya matunda," alisema Mtaka.

Mkuu huyo wa mkoa aliagiza kila mtu ambaye atashiriki katika upandaji miti kuhakikisha anautunza ili usife na kufanya jambo hilo kukosa tija.

"Kila mmoja wetu lazima apande mti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kila mwenye kiwanja chake ahakikishe anapanda miti. Mtu asiende kutembelea kiwanja chake kama anakwenda kuona mgonjwa. Panda miti ili hata ukianza ujenzi ukute tayari miti ya kivuli na matunda ipo," alisema Mtaka





# Ujenzi minara 42 kuimarisha mawasiliano katika shehia 38

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MFUKO wa Mawasiliano kwa Wote Tanzania (UCSAF) na kampuni ya simu za mkononi ya ZANTEL, zimetiliana saini mkataba wa mradi wa ujenzi wa minara 42 katika shehia 38 za Zanzibar ili kuimarisha huduma za mawasiliano.

Mkataba huo ulitiwa saini jana na Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Justina Mashiba, na Ofisa Mkuu wa Fedha wa ZANTEL, Aziz Said Ali, na kushuhudiwa na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi wa Zanzibar, Rahma Kassim Ali, na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye.

Hafla hiyo ilifanyika makao makuu ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Kisauni mjini Zanzibar.

Ujenzi huo wa minara 42 unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 6.9 na kuvifikia vijiji 38 vya Zanzibar huku Serikali ikiwa na mpango wa kuvifikia vijiji 2,116 Tanzania nzima.

Akizungumza kabla ya utiaji saini wa makubaliano hayo, Waziri Nape alisema serikali zote mbili zinakusudia kuimarisha huduma za mawasiliano nchi nzima ili wananchi wanufaike na kasi ya mawasiliano.

Nape alisema huduma za mawasiliano ni muhimu katika kasi ya ukuaji ya maendeleo ya uchumi na UCSAF itahakikisha pande zote mbili za Muungano zinanufaika na huduma hizo.

Alisema kutokana na kukua kwa sayansi ya teknolojia, ni vyema serikali ikawekeza nguvu katika kuboresha na kuimarisha huduma hiyo muhimu ili kwenda sambamba na nchi zilizoendelea.

Pia alizitaka taasisi zinazotoa vibali vya ujenzi, kupunguza urasimu katika utoaji wa vibali hasa katika miradi ya serikali ili kuhakikisha ujenzi huo wa minara usiwe wa kusuasua. Naye Waziri Rahma alisema utiaji saini huo ni mwendelezo wa mpango wa kuboresha mawasiliano katika sehemu maalumu zilizoainishwa kuwa na changamoto za mawasiliano.

Waziri huyo aliitaka UCSAF kutosita kuwasiliana na wizara iwapo kutakuwa na kikwazo chochote kitakachosababisha kuchelewesha kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huo.

Mashiba alisema bado vijiji vingi havijafaidika na huduma za mawasiliano kutokana na kutofikishiwa huduma hiyo, hivyo serikali chini ya mfuko wa mawasiliano kwa wote, ina mpango wa kuvifikia zaidi ya vijiji 2,000 ili navyo vifaidike na huduma ya mawasiliano.

Mtendaji huyo alisema tangu kuanzishwa kwa UCSAF na kuanza kwa miradi, kuwekuwa na ukuaji mkubwa wa maeneo yanayofikiwa na mawasiliano ya simu za mkononi hasa maeneo ya vijijini.

Alisema kwa sasa asilimia 94.5 ya watu nchini waafikiwa na huduma za mawasiliano ya simu ikilinganishwa na asilimia 45 tu mwaka 2006 kipindi UCSAF inaanzishwa.

"Hadi kufikia Disemba 2021, Serikali kupitia UCSAF imetia saini mikataba 41 ya huduma za mawasiliano ya simu katika kata 1,068 zenye takribani vijiji 3,297 vyenye wakazi wapatao 12,981,164," alisema.




Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (wa tatu kushoto waliosimama) na Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Rahma Kassim Ali (wa nne kushoto waliosimama), wakishuhudia wakati Mtendaji Mkuu wa mfuko wa mawasiliano kwa wote (UCSAF), Justina Mashina na Ofisa Mkuu wa Fedha kutoka kampuni ya Zantel, Azizi Said, wakitia saini mkataba wa ujenzi wa minara 42 ya mawasiliano, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## SMZ yaahidi ushirikiano wa afya na KMKM

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, ameahidi kuendeleza ushirikiano wa karibu na Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) katika sekta ya afya ili kutoa huduma bora kwa jamii.

Mazrui aliyasema hayo jana alipotembelea hospitali ya KMKM iliyoko Kibweni, mjini Zanzibar.

Alisema kutokana na umuhimu wa hospitali hiyo, kuna haja ya kufanya jitihada za kuipandisha hadhi kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa na kuwa hospitali ya mkoa.

Waziri alisema jitihada za KMKM za kuwekeza katika miradi mbalimbali, ikiwamo sekta za uvuvi na afya, ni jambo zuri ambalo litasaidia kuleta maendeleo nchini.

Pia alikitaka kikosi hicho kutokurudi nyuma katika kufikia malengo kiliyojiwekea na dhamira yake ya kutaka kuleta maendeleo katika nchi, jambo linalosisitizwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi.

Mkuu wa Kikosi cha KMKM, Komodoo Azan Hassan Msingiri, alisifu uamuzi wa waziri kutaka kuzitatua changamoto za hospitali ya KMKM kwa sababu asilimia kubwa ya huduma zinazotolewa ni kwa raia wa kawaida.

Mkuu huyo aliiomba Wizara ya Afya kuiongezea dawa hospitali hiyo ili jamii inufaike na huduma inayotolewa.

Akielezea matarajio ya hospitali hiyo Daktari Mkuu Mwashamba Mbarouk alisema ni pamoja na kuongeza idadi ya madaktari, vifaa tiba na dawa ili kutoa huduma bora kwa jamii.

Dk. Mbarouk alisema kikosi hicho kimejipanga kuanzisha bohari kuu ambayo itauza dawa katika visiwa vya Unguja na Pemba.

# Ujenzi wa bandari ya Malinzi sasa wanukia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi ameshuhudia utiaji saini mpango mkuu wa kufanya utafiti na upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya Malindi ambayo itakuwa ya kitalii pamoja na mji wa kisasa katika eneo la Bwawani mjini Zanzibar.

Utiaji saini huo ulifanyika juzi Ikulu Zanzibar huku Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) ikiwasilishwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Amour Hamil Bakari.

Upande wa Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman uliwakilishwa na Sheikh Nasser al Harthy ambaye alitia saini sambamba na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Bandari, Nahaat Mahfoudh, akifanya hivyo kwa niaba ya Zanzibar.

Akizungumza baada ya utiaji saini huo, Rais Dk. Mwinyi alisema kwamba katika mradi huo bandari mpya ya Malindi ambayo inatarajiwa kujengwa baada ya kujengwa bandari ya mpya ya makontena, Mangapwani, itageuzwa kuwa bandari ya kitalii pamoja na kulitengeneza eneo lote kutoka bandarini Malindi hadi Hoteli ya Bwawani ili eneo hilo liwe na majengo mapya ya burudani, hoteli na majengo ya makazi.

Alisema kuwa eneo hilo ambalo litakuwa la mji mpya wa kitalii lina kisiwa kuwa na ukubwa wa hekta 30 ambazo zitatokana na kufukia bahari.

Dk. Mwinyi alisema amefurahishwa kutokana na hatua zinazochukuliwa na serikali katika kutafuta wawekezaji katika maeneo mbalimbali. Serikali ya Oman, mbali na kutiliana saini na serikali juu ya ujenzi wa bandari ya makontena pia imetiliana saini ujenzi huo utakaowezesha kuwa na mji mpya wa kisasa eneo la Malindi.

Rais Dk. Mwinyi alitoa shukrani kwa kujitokeza kwa wawekezaji hao na kusema Dola milioni 500 zitatumika katika ujenzi wa mradi huo mkubwa wa kimkakati.

Alitumia fursa hiyo kuwapongeza wawekezaji hao waliokuwa na nia ya kuwekeza Zanzibar na kusema Zanzibar inaendelea kutafuta wawekezaji kwa kuwa mpango wa maendeleo ya Zanzibar wa miaka mitano unatakiwa kushirikisha sekta binafsi katika kusaidiana na serikali kujenga miradi ya maendeleo yenye tija na ya kibiashara.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, alisema ujenzi wa mradi huo utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuiletea mendeleo endelevu Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uwekezaji ya Oman, Sheikh Mohamed Al Taooqi alisema kwamba mamlaka hiyo itahakikisha mradi huo unafanikiwa na kufikia malengo yaliyokusudiwa.



**ROSE**

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE





# HANA BAHATI? au Shilole hana nyota

KIZA kimetanda tena katika maisha ya mapenzi ya mwanamuziki na mjasiriamali, Zuwena Mohamed, maarufu kama Shilole, baada ya hivi karibuni kuibuka uvumi kwamba ameachwa na mume wake Rommy.

Bado utata unaongezeka kuhusu suala hilo, baada ya Shilole kuwa kimya kuelezea hatma ya ndoa yake.

Wakati watu wakijadili kwa kina kwa nini msanii huyo amekuwa hana bahati na wanaume, mwenyewe ameibuka na kuweka picha katika ukurasa wake wa Instagram, ikionyesha yupo na mume wake Rommy wakipeana mahaba kemkem.

Shilole ameamua kuweka picha hiyo kama ujumbe tosha kwamba ndoa yake bado iko imara.

Picha hiyo imeonekana kuwagusa wafuasi wake wengi ambao walikuwa na maoni tofauti, huku idadi kubwa wakimpongeza kwa kuwa mwanamke jasiri anayelinda penzi lake kwa nguvu zote.

Hata hivyo, kuna baadhi wanahoji kwa nini katika picha zake za hivi karibuni hayupo na mume wake, badala yake anakuwa na watu wengine tofauti na ilivyokuwa zamani.

Rommy ni mume wake wa tatu, lakini katika maisha yake wanaume wake ambao wamekuwa maarufu ni Nuh Mziwanda na Ashraf Uchebe.

BASI SAWA

## Rose hukuwaza zamani, iweje sasa?



MWANAMUZIKI mkongwe wa Injili, Rose Mhando, sasa anawaza kuwa na ndoa, lakini hataki mume kutoka Afrika na badala yake awe mzungu.

Rose aliyetamba na wimbo wake wa 'Utamu wa Yesu' , amesema kupitia ukurasa wake wa Instagram kwamba licha ya kuwa mzungu, pia awe na kitita cha pesa.

"Yesu nitendee, ombi langu mwaka huu nataka nipate mume mzungu na mwenye hela". Ameandika.

## Ommy Boi awaambia 'Haitoshi' kucheza



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, OmmyBoi_akimshirikisha mkali Belle9, ametambulisha ngoma yake mpya inayoitwa 'Haitoshi' ambayo imeanza kuwashika mashabiki wa muziki.

Ngoma hiyo, imetayarishwa na prodyuza Lamcukie_ huku video ikiongozwa na Kilonzo.

"Nawaomba mashabiki zangu kuniunga mkono katika wimbo wangu ambao umeandaliwa kwa ajili yao, natumaini mtafurahi na kukidhi kiu yenu kwani ujumbe wake unatosha kukufanya utafakari kwa kina," amesema.



## MC Pilipili kuzindua kanisa kesho

MSANII wa vichekesho Emmanuel Mathias, maarufu kama MC Pilipili, ameanzisha kanisa lake liitwalo Kanisa la Upendo ambalo anatarajia kulizindua rasmi kesho Jumapili.

MC Pilipili kwa sasa ni mchungaji wa kanisa hilo, amesema katika uzinduzi huo amealika waimbaji mbalimbali wa nyimbo za Injili akiwamo nyota wa nyimbo hizo Ambwene Mwasongwe.

"Ninajua kwamba watu wengi wananifahamu kutokana na umaarufu wangu niliopata kupitia sanaa, lakini kwa sasa mimi ni Mchungaji wa Kanisa la Upendo au Love Church," amesema MC Pilipili.

Amesema, kila mwenye upendo anaalikwa kushiriki kwenye ibada ya uzinduzi wa kanisa lake ambalo halibagui mtu dini au kabila, bali kinachohimizwa ni upendo miongoni mwa jamii.

## Pretty Girl: Mapenzi kizunguzungu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine tabia ya mtu inatokana na sehemu aliyotokea, mazingira yaliyomzunguka au tukio lililomtokea zamani na kumuathi kisaikolojia.

Unaweza kukutana na wanaume ambao hawataki kabisa wanawake, au hataki kuoa, kumbe huko nyuma alishawahi kukutana na maswahibu.

Hata wanawake ni hivyo hivyo, Unamkuta hataki mwanaume au kuolewa. Matukio haya yanawafanya kuathirika kisaikolojia na kila anayekutana naye anaona ni wale wale tu.

Mtunzi wa filamu ya 'Pretty Girl' ana mtazamo huo. Ni filamu iliyochezwa na Vicent Kigosi maarufu kama Ray, Mohamed Mwikongi maarufu kama Frank, Hashim Kambi, Hassan Moshi au Tx Junior, Salma Jabu 'Nisha', Irene Uwoya, Tino Muya na wengineo.

Irene ni bosi kwenye kampuni moja hivi. Lakini pamoja na kuwa mwanamke ambao wengi wao wana huruma, lakini amekuwa na tania ya ukali, akinyanyasa wanafanyakazi wake, hasa wa kiume.

Baada ya muda mrefu, ukali wake unasababisha kampuni kuanza kufilisika taratibu kutokana na uongozi mbovu.

Ray, kijana tajiri, anaamua kuwekeza kwa kununua hisa na kuifanya kampuni kuinuka upya.

Hata hivyo bosi anaendelea kuwa yule yule Irene.

Bodi ya Wakurugenzi inakutana kwa nia ya kutatuta tatizo. Baada ya majadiliano inagundulika kuwa bila Irene kuondoka, kampuni hiyo itaendelea kufilisika au kulegalega.

Ray na jopo lake la Wakurugenzi wanajadili tatizo la Irene na kugundua kuwa ameathirika kisaikolojia.

Anatafutwa daktari kwa ajili ya kutatua tatizo lake, lakini mwenyewe anapinga na kusema kuwa hana jambo lolote linalomsibu na wala haumwi.

Kampuni sasa inamlazimisha kwa nguvu afanye hivyo. Inampeleka kliniki. Hatimaye inagundulika kuwa ni kweli alikuwa na matatizo yaliyotokana na ukatili kutoka kwa mumewe hapo zamani.




Kumbe huko nyuma, alilazimishwa na wazazi wake kuolewa na mwanaume asiyempenda. Na mume kumbe naye alikuwa hampendi.

Ndani ikawa tafrani. Akawa anamletea mkewe wanawake wengine ndani. Irene anapokwenda kwa wazazi wake anarudishwa kwa mumewe.

Hali ilikuwa mbaya zaidi mume alipomkodishia vijana wa kihuni ili wambake kwa sababu hampendi na hataki kuondoka.

Irene akamwambia daktari kuwa hiyo ndiyo sababu iliyomfanya awe na tabia hiyo ya kuwa mkali na kuwachukia ovyo wanaume.

Pamoja na yote hayo, kijana tajiri mwenye hisa nyingi kwenye kampuni hiyo, Ray anamwambia Irene afute historia yote ya nyuma, kwani tangu alipomuona kwa mara ya kwanza alitokea kumpenda kwa dhati na anataka kumuoa, ili kumfanya awe mtu mpya na kusahau madhila yote.






## DJ Sippy afikiria kuwekeza Bongo

KUTOKA nchini Marekani mprodusya mkali Patrick Sippy 'DJ Sippy', hatimaye ametua Bongo kwa lengo la kuwekeza na kukutana na wadau wa muziki.

Akizungumza na BT, Meneja wa Handzdown Records, Lonely Nzali, amesema Dj Sippy ambaye ni bosi wa lebo hiyo amekuja Tanzania kuangalia fursa mbalimbali za kuwekeza kwenye sanaa.

"Dj Sippy atakuwepo hapa Tanzania mpaka mwisho wa mwezi huu, lengo lake ni kuangalia fursa mbalimbali ili aweze kuwekeza hapa nyumbani, kama tunavyojua yupo nyuma ya wasanii wengi wanaofanya vizuri kama rapa wa kike Trixy Tonic na Rasco Sembo," amesema Nzali.

## MASTAA WA 'MUVI' KIBOKO YA MANINJA

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE miaka ya 1980 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000, Wabongo walikuwa hawashikiki kwa 'muvi' mbalimbali, zikiwemo za Kizungu, Kihindi, Kijapani na Kichina.

Filamu za Kihindi walipenda zote za mapigamo na mapenzi, lakini kwa hizo zilizobaki walipenda za kimapigano na kibabe.

Kati ya hizo kuna za kivita, sanaa ya mapigano, kama kung-fu ya Bruce Lee, karate na staili zingine mbalimbali.

Lakini moja ya aina ya mapigano yaliyokuwa yameshangaza na kupendwa na wengi ni ya kininja.

Filamu za kininja zilijizolea mashabiki wengi miaka hiyo kutokana na staili yake ya wapiganaji wake ambao walionekana kama si watu wa kawaida, kwani walikuwa wepesi wa kila kitu, kuruka, kupanda juu, na hata wakati mwingine kupotea kimiujiza.

Walikuwa na uwezo wa kupigana kwa mikono na zana mbalimbali za kijadi. Huwa hawatumii bastola tu. Asili ya staili hii ni nchini Japan.

Pamoja hayo kulikuwa na 'mastelingi' ambao walikuwa ni kiboko yao. Yaani hao kwenye filamu hizo walikuwa wakiwashinda maninja na hila zao zote.

Hawa ni baadhi ya mastaa wa filamu ambao walikuwa ni kiboko ya majina.

**Michael Dudikoff**

Huyu ni 'stelingi' Mmarekani ambaye alitamba sana miaka ya 1980 na filamu zake kali za maninja, na hasa alipotoa kwa mara ya kwanza picha ya kwanza American Ninja mwaka 1985.

Filamu hiyo ilifuatia tena na mfululizo wa American Ninja namba mbili na kuendelea na kumpatia umaarufu mkubwa sana.

Kwa watazamaji wa picha wa wakati huo Bongo, wanamtazama staa huyu kuwa ni mmoja wa waliokuwa kiboko wa maninja, kwani pamoja na hila zao zote, lakini alikuwa akiwafyeka.

Kwenye picha alikuwa akicheza kama Mmarekani aliyepata mafunzo ya Kininja na babu mmoja wa Kijapani akiwa mdogo, na baadaye kuja kuwatesa 'Wajepu' wenyewe na 'Wavete' yaani Wavietnam.

**Alexander Low**

Huyu ni bingwa wa zamani wa sanaa za mapigano staili ya 'taekwando' wa Taiwan. Huyu naye ni mtaalamu wa kuwaduwaza maninja. Ni kiboko wa maninja. Amecheza picha mbalimbali kama vile The Ninja Hunter, The Super Ninja, Ninja vs Shaolin na nyingine nyingi.

Kama alivyo Mmarekani Dudikoff, huyu naye alikuwa kipenzi cha mashabiki wengi wa filamu wakati huo, kutokana na uhodari wake wa kuwatwanga maninja ambayo wanachukuliwa ni watu katili na wakorofi kwenye 'muvi'.

**Sho Kosugi**

Huyu sasa ni ninja halisi. Wakati hawa wengine wakicheza kama filamu tu, lakini Sho Kosugi ni ninja hasa na Mjapani, kule kule kulikotoka mchezo huo. Anacheza michezo yote ya sanaa za mapigano, kama karate, kendo, judo, laido, kobudo, aikido na ninjutsu ambayo ndiyo staili wanayojifunza zaidi maninja. Jamaa ni bingwa wa zamani wa karate nchini kwao.

Kwa sasa anatengeneza filamu na kufundisha, lakini naye alikuwa ni mtaalamu kwa kuwatengeneza maninja kwenye filamu zake nyingi alizocheza na Wabongo wanamfahamu zaidi kwa jina la 'Shokoshugi'.

**Franco Nero**

Ni mastaa wa mwanzo kabisa kucheza filamu za kininja. Jamaa ni Mtaliano, lakini alicheza filamu chache za kininja, ikiwemo Enter the Ninja, iliyotoka mwaka 1981. Ni mmoja wa mastaa ambao hawaimbwi sana kama wenzake hapa Bongo, lakini wale wenye kufutilia sana filamu za mapigano wanamfahamu sana na kumkubali mbabe huyu.

**Jet Li**

Wala sina haja ya kumuelezea sana mbabe huyu kwani hata watoto wadogo leo hii wanamfahamu.

Staa huyu, mbali na kucheza filamu nyingi, lakini pia hakuacha baadhi ya filamu zake kupambana na maninja.



# Ka3na ona unavyotaka kuleta balaa

MSHIRIKI wa zamani wa Big Brother Naija, Ka3na, ameamua kuweka wazi kwamba ndoa yake na mume wake Jones, imevunjika rasmi.

Akitumia ukurasa wake wa Twitter, mrembo huyo amesema kuanzia sasa ataendelea kumheshimu na atabaki tu kuwa mume wake wa zamamani.

"Mdio kwa sasa nipo singo, sihitaji kurudi nyuma naamua kuweka wazi mtandaoni ili kila mtu afahamu na niwe huru. Jones atabaki kuwa mume wa zamani na baba wa watoto wangu pekee," amesema.



## Dj Cuppy hamkubali kabisa Kanye West

DJ maarufu nchini Nigeria, ambaye anajulikana kama DJ Cuppy. Ameibua mjadala mkali baada ya kumshutumu rapa wa Marekani Kanye West, kwamba ni tajiri namba moja kwa watu weusi.

Akitumia Twitter, Dj Cuppy, amesema mwanamuziki huyo hawezi kumpita bilionea kutoka nchini humo Aliko Dangote, ambaye ana msururu wa makampuni sehemu mbalimbali Afrika..

"Sikubaliani kwamba Kanye West kuwa ndiye tajiri kupita watu wote weusi, nafikiri tumwambie ukweli kuwa sio tajiri kumpita Aliko Dangote, lazima tuweke sawa jambo hili," ameandika.

## Duncan sasa inatosha, ukizidi utaumia

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Duncan Mighty, anatuhumiwa kukimbia na kiasi cha Naira milioni 3.6 kama malipo ya kushiriki tamasha la muziki.

Jackson Ude ambaye ni muandaaji wa tamasha hilo, amesema mwanamuziki huyo alitakiwa kushiriki tamasha hilo la vijana na alilipwa kiasi hichi cha pesa, lakini hakutokea jukwaani.

"Nilimlipa Duncan Mighty naira milioni 3, kwa ajili ya tamasha la vijana la Nkporo lilofanyika Desemba 30, lakini hakutokea katika shoo, nilimtafuta sikumpata na hata simu yangu hapokei," amesema Ude.





## Kylie aongoza kwa wafuasi duniani

MWANAMITINDO na mshiriki wa kipindi cha maisha nchini Marekani, Kylie Jenner, amefanikiwa kuvunja rekodi ya kuwa mwanamke wa kwanza kuwa na wafuasi milioni 3 katika mtandao wa Instagram.

Mrembo huyo bilionea amekuwa maarufu kutokana na kuwa katika familia ya Kardashian, ameshika nafasi hiyo huku akifuatiwa na Ariana Grande.

Katika ripoti hiyo, nafasi ya tatu inashikiliwa na staa wa muziki Selena Gomez ambaye ana wafuasi milioni 289.

## Card B umefanya jambo kubwa

RAPA nyota wa Marekani Cardi B, ameahidi kulipia gharama za mazishi ya wahanga wote wa tukio la moto lililotokea jijini New York.

Moto mkali ulikumba jumba la ghorofa la vyumba 120 huko Bronx, New York, mapema mwezi huo na kuua wakaazi kadhaa wakiwemo watoto.

"Siwezi kuanza kufikiria uchungu ambao familia za marehemu wanapitia, lakini ninatumai kuwa kutokuwa na wasiwasi juu ya gharama zinazohusiana na kuzika wapendwa wao, nitasaidia wakati wengine wanasonga mbele na matibabu," Cardi B aliiambia TMZ.



MAKALA

# Wanahabari wanawake wanapojizatiti kidigitali



Matumizi ya mitandao ya kijamii kwa waandishi wanawake inaleta tija katika mawasiliano ya habari

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI dunia ikisonga mbele kiteknolojia, wanawake hawajaachwa nyuma katika kwenda sambamba na mapinduzi ya kidigitali.

Katika kuona kundi hilo linakwenda kwa kasi kama dunia inavyohitaji kwa sasa, wanahabari 60 wanawake kutoka mikoa tofauti wamepewa mafunzo ya kukuza ujuzi kidigitali kupitia taaluma yao.

Lengo kubwa hapa ni kuona wanawake wanapata uwezo wa namna ya kuandika habari zinazosheheni data na matumizi sahihi ya mitandao.

Mafunzo hayo wamepata kupitia mpango wa Women At WebTZ, uliowezeshwa na taasisi ya Boresha Habari kupitia Shirika la Misaada la Marekani (USAID) nchini Tanzania.

Zahara Tunda ambaye alikuwa mkufunzi anasema uandishi wa kidigitali huwa unakuwa na namna tofauti na ule wa zamani, hapa mwandishi anatakiwa kutumia michoro, picha na maumbo tofauti ili kumvutia msomaji katika makala au habari iliyochapishwa au kurushwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Badala ya kuandika namba kwenye habari yako, mwandishi unatakiwa kuwa mbunifu kwa kutumia vielelezo, michoro, ambavyo vinatafsirika haraka kwa msomaji. Mara nyingi watu huogopa namba zenye tarakimu nyingi, lakini 'graph' itasaidia kupunguza woga," anasema Tunda.

Naye Mkufunzi Lily anasema kila mwandishi anayetamani kuwa kidigitali ni lazima awe na uwezo mzuri wa mawasiliano, fikra pana na kuwa na wazo la kutoa suluhisho la haraka kupitia uandishi.

"Unaweza kujua namna ya kukusanya taarifa kutoka vyanzo mbalimbali hasa mitandao ya kijamii uwe nayo karibu kwa kufahamu kinachopendwa kwa wakati gani. Tambua namna bora na mbinu za uandishi wa data na kuhusisha habari zako mtandaoni kwa sababu ulimwengu ni kidigitali zaidi," anasema Lily.

**MPANGO ULIOPO**

Mpango wa mradi wa Women At Web project unaosimamiwa na Media Convergency, umelenga kuhakikisha wanawake waliopo mijini na nje ya mji wananufaika na mabadiliko ya kidigitali.

Nchi zilizomo kwenye mradi huo ni Uganda, Kenya, Tanzania na Rwanda.

Lengo la mradi huo ni kuwapa ujuzi wa kidigitali hususan wanawake vijana ambao watafanikiwa kukabiliana na ukatili wa kijinsia mtandaoni kwa kutoa taarifa mbalimbali.

Mitandao ya kijamii, inaongoza kuwa na watumiaji wengi hasa kupitia instagram, facebook, whatsapp, YouTube, na mingineyo huku ikikadiriwa watumiaji wa huduma hiyo wanafikia bilioni 3.8. Pia inaaminika ni moja ya njia ya mawasiliano inayofikia watu kwa haraka duniani kote.

**WANAWAKE NA DIGITALI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Zaina Foundation, Zaituni Njovu akizungumza kwenye moja ya mafunzo hayo, anasema katika kazi za kidigitali ni muhimu kulinda vifaa vya kazi pamoja na kuzingatia usahihi wa vyanzo vya habari.

Zaituni anasema lengo ni kuwawezesha wanawake kwa kuwapa ujuzi wa namna ya kuhakikisha usalama katika matumizi ya mtandaoni kwenye dunia ya kiteknolojia, ikizingatiwa wanawake ni kundi kubwa ambalo bado halijahusishwa kikamilifu.

"Haki ya kupokea, kutuma na kutoa taarifa ni ya kila mmoja. Lakini tunahitaji kuwepo usalama wa matumizi ya mtandao, kulindwa kwa faragha, kwa kuwa wanawake ni kati ya waathiriwa wakubwa wa picha zisizo na maadili zikisambazwa mitandaoni bila mtu kujua," anasema Zaituni.

Anasema mteja anayejiunga na huduma za mtandao ana haki ya kulindwa usalama wake, kupata huduma ya uhakika bila kukatika na iwapo inatokea tatizo la kiufundi, taarifa itolewe kwa mtumiaji.

"Mtumiaji ameamua kujiunga na kifurushi cha siku au hata wiki, lakini baada ya muda unaambiwa mtandao wa kampuni fulani haupatikani bila taarifa yeyote. Ni haki yako kupata taarifa, wakati wowote," anasema.

Anafafanua kwamba mafunzo hayo ambayo ni ya awali kutolewa kwa wanahabari, yanawaongezea ujuzi wanahabari, ili kukabiliana na changamoto zilizopo mtandaoni pamoja na kujiongezea fursa za kiuchumi.

"Tunawaelimisha wanawake katika matumizi ya teknolojia na mtandao, wakati wigo ukikua kila saa, hivyo ipo haja ya kuwa makini na matumizi ikiwamo kuvamiwa na wadukuzi na kuvujisha siri zako," anasema Zaituni.

**IDADI YA WATUMIAJI**

Zaituni anasema takwimu duniani zinaonyesha idadi ya watumiaji wa mtandao imeongezeka na kufikia watu bilioni 4.5 na kati yao watumiaji milioni 23 ni kutoka Tanzania.

"Wakati matumizi yakikua duniani muda wa kuongeza usalama wa kimtandao kwa mtumiaji unahitajika kwa kuwawezesha namna ya kuweka usiri wa taarifa zao na data zao," anasema Zaituni.

**CHANGAMOTO MTANDAONI**

Zaituni anasema zilizopo katika mtandao kuna usalama mdogo huku wanawake kadhaa wakiwa na elimu ndogo.

"Changamoto ni elimu kwa ambao wanatakiwa kufikisha habari kupitia mtandao, ili kutoa taarifa sahihi kuelimisha umma kipindi ambacho ulimwengu unahitaji elimu zaidi," anasema.

Anaeleza kutokana na watu wengi kuwa na elimu ndogo imekuwa ni vigumu kulinda taarifa.

## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Kumbuka mbwembwe, haiba na visa vya wakuu wa shule zama hizo

Na Adam Fungamwango

MIAKA ya hivi karibuni Walimu Wakuu wa Shule za Sekondari wanaonekana kuchukuliwa au kujichukulia poa tu, labda kutokana na mazingira ya sasa yanatofautiana na ya zamani, lakini miaka ya zamani walikuwa wakiogopwa na kuheshimiwa sana mithili ya wabunge au mawaziri kiasi kwamba, hata baadhi ya wanafunzi walikuwa wakitamani kuwa kama wao.

Si shuleni wala mitaani, wakuu wa shule walikuwa wakiheshimika na kujulikana kila wanakopita, watu wote wanakuwa wajua huyu ni nani, ukiongeza na mavazi yao, kwani wanaume walipenda sana kuvaa suti, ndiyo kabisa.

Nakumbuka kuna mwanafunzi mmoja alikuwa akimuiga mwalimu mkuu wa shule fulani miaka ya nyuma, akiwa na sauti na utembeaji, amini usiamini baada ya miaka mingi kupita naye akaja kuwa mkuu wa shule.

Awe mwanaume au mwanamke, walikuwa na tabia zinazofanana jinsi walivyokuwa wakiongoza.

Miaka ya 1990 kurudi nyuma, kulikuwapo shule za sekondari maarufu kama Azania, Tambaza, Ilboru na Jangwani za Dar es Salaam.

Pia, Tabora kulikuwapo sekondari za Tabora Boys na Tabora Girls, ilhali Kilimajaro kulivumishwa na Weruweru, Umbwe, pia Moshi Ufundi; mkoani Pwani ni Kibaha, Bagamoyo na Minaki; mkoani Morogoro kuna orodha kama za Kilakala na Mzumbe.

Dodoma nako si haba, kunatajwa Msalato na Mazengo; Ruvuma kuna Songea Boys na Songea Girls, Iringa kama kawaida magwiji Ifunda Ufundi na Malangali, majirani zao kuna Mbeya Day na dada zao wa Loleza; Sumbawanga kuna Kantalamba, Mtwara Ufundi huko Kusini, Bwiru Boys na Bwiru Girls, Mwanza; Musoma Sec; na Rugambwa mkoani Kagera.

Kwa kawaida shule zilikuwa zinaendeshwa na makamu wa wakuu wa shule, walimu wa vitengo na viranja ambao baadhi walikua wanachaguliwa kidemokrasia na wengine kuteuliwa na jopo la walimu kutokana na uwezo na nidhamu zao na walikuwa wanaheshimika na wakuu wa shule, walimu na wanafunzi wenzao.

Huwezi kumkuta mkuu wa shule anamdhalilisha kiranja hadharani, achilia mbali walimu wake

katika mgawanyo huo wa walimu, jambo ambalo kila mwalimu kuanzia wanafunzi wa zamani wa zama hizo, huenda hata mpaka wa leo, wanawafahamu fika.

Mengi yalimalizwa na wanaoitwa walimu wa darasa na mwalimu wa nidhamu. Maana hao ndiyo wanaopambana na wanafunzi, kila kukicha kwenye maisha ya shule, kuanzia uchelewaji, kufanya vibaya darasani na vipengele kibao vya ukorofi, maana nasi wanafunzi wa siku hizo, tukikumbuka maisha yetu, tulikuwa hatushikiki:

Maana kitabia tulikuwa 'hatujambo', ukikosekana kwa kosa hili, utapatikana na lile. Maisha yetu na walimu yalikuwa kama ya mhalifu na askari, ila tofauti yake kuna wakati yalibeba sura ya pili, kama ya mtoto na mwana.

Sasa sisi na hao walimu wetu, hata mabosi wengine kuanzia watumishi wa shule na viranja, tuliwajibika chini ya mtu ambaye wa kipekee kabisa, aitwaye Mkuu wa Shule.

Kwanza kumuona tu alikuwa adimu, pia anapoonekana na haiba yake, vazi la kiafisa, iwe kaunda suti, au ngwabi, hapo hujasahau kuna siku ndani ya tai, nguo zimekubali pasi kisawasawa na mwendo wa mbwembwe, hapana shaka iko wazi kabisa ni mtawala mkuu wa hiyo himaya.

Sasa usithubuti kuchokoza Kiingereza kinachoshuka mdomoni humo. Sifa ya ziada, bila ya kujali idadi yenu anamjua kila mwanafunzi kwa majina kamili, tabia, wazazi na mwenendo, we acha tu!

Sifa yao kubwa ni kuonekana kwa nadra. Haonekani hovyo hovyo, sana sana kwenye mambo makubwa tu. Siku akija kuongea na jumuiya ya shule yaani walimu, wanafunzi na wafanyakazi wengine ataongelea mwelekekeo wa shule kiujumla kitaaluma, nidhamu na mikakati mbalimbali.

Huwezi kukuta anazungumzia mambo ya safari, sijui wanafunzi wanakwenda kutembelea wapi, sijui darasa gani linapiga kelele au nani sijui hajasafisha eneo lake. Hata kama kuna wakosaji wa kuadhibiwa basi huwa ni zile adhabu kubwa tu.

Rafiki yangu mmoja aliyesoma Ifunda, aliniambia kuwa wakati anasoma mkuu wao alikuwa ni Mwinuka, yeye hata siku moja, hapendi kuongea na wanafunzi isipokuwa kuna jambo nyeti, au shule inafungwa.

Jamaa mmoja akaniambia kuwa mkuu wao wa shule alikuwa akipiga suti za uhakika mithili ya mbunge au waziri na hawakujua alikuwa anazitoa wapi suti hizo kali, zenye ubora wa hali ya juu kipindi kile.

"Siku akipanda watu wote kimya kabisa, sijui yule baba miaka ile ya 1970 mwanzoni suti alikuwa anazitoa wapi, maana kila siku suti mpya. Kwanza, kumuona tu ilikuwa si kawaida, kengele ikigongwa akisimama mnajua kabisa kuna kitu kikubwa," anasimulia mwanafunzi mmoja wa zamani ambaye kwa sasa ni mtu mzima sana.

Labda kutokana na mabadiliko ya wakati, kwa sasa hawatishi tena kama zamani, inawezekana ni kwa sababu wengi wao wanapenda kuongea kila kitu, kila wakati kiasi kwamba wanakosa mvuto, pia kwa sasa wengi wao hawana umri mkubwa sana kama wale wa zamani, hawana mbwembwe zile za 'kikoloni' hata mavazi yao wako 'simpo' tu.

Sms: +255 716 350534



Sehemu ya haiba ya mavazi na utanashati waliouhusudu wakuu wa shule wa zamani. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**



Sehemu ya majengo la Shule ya Sekondari Old Moshi, iliyopo mjini Moshi, tangu zama za ukoloni wa Kijerumani nchini.

## Jeshi lateua mawaziri wake

**KHARTOOM,** SUDAN

MKUU wa Jeshi la Sudan, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, amewateua mawaziri 15 katika serikali mpya ya mpito ambayo inapingwa na wananchi.

Uteuzi huo ni baada ya miezi mitatu tangu walivyofanya mapinduzi na kuiondoa madarakani serikali ya mpito na kusababisha kukwama kwa mpango wa mpito kuelekea uchaguzi.

Tangu mapinduzi hayo kumekuwa na maandamano makubwa ya mara kwa mara ambayo yameshuhudia waandamanaji zaidi ya 70 wakiuawa na vikosi vya usalama.

Waandishi wa habari walisema kutajwa kwa serikali hiyo mpya hakuwezi kuwaridhisha waandamanaji wanaotaka wanajeshi waondoke katika ulingo wa kisiasa.

Hapo awali, majaji nchini humo walitaka uchunguzi ufanyike kuhusu ukandamizaji unaofanywa dhidi ya waandamanaji, wakiwashutumu viongozi wa kijeshi kwa kutekeleza ukiukaji huo wa haki za kibinadamu.

Marekani imerejea msimamo wake wa kutorudisha msaada wa kiuchumi kwa Sudan, isipokuwa tu kutakapokuwa na usitishaji wa ghasia na serikali inayoongozwa na raia kurejeshwa.

**BBC**

## Waziri akana kuomba msamaha kwa rais

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

WAZIRI wa Utalii wa Afrika Kusini, Lindiwe Sisulu amekataa kuomba msamaha kwa rais kwa ukosoaji wake wa mahakama.

Hatua hiyo imekuja kufuatia taarifa ya Ikulu kueleza kuwa Rais Cyril Ramaphosa, alikutana na Sisulu wiki hii na aliomba msamaha na kufuta maoni yake ya kuumiza.

Hata hivyo, Sisulu alisema hajaomba msamaha na kusisitiza ilikuwa ya upotoshaji kuhusu mkutano aliofanya na kiongozi huyo.

Alisema alisimamia matamshi yake, hakuomba msamaha na kwamba yaliyomo katika taarifa ya rais ni ya kusikitisha.

Katika mahojiano na Shirika la Utangazaji la Serikali SABC, msemaji wake Steve Motale, alisema zaidi waziri huyo alitarajia mazungumzo zaidi na Rais Ramaphosa na alishtushwa na taarifa hiyo.

Katika makala iliyochapishwa majuzi na vyombo vya habari, Sisulu aliandika kwamba baadhi ya majaji walikuwa Waafrika waliotawaliwa kiakili.

Pia alisema katiba imeshindwa kuboresha maisha ya watu weusi wa Afrika Kusini wanaoishi katika umasikini. **BBC**

# Ukraine yashutumu msimamo wa Marekani

**KIEV,** UKRINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, ameshutumu matamshi yaliyotolewa na Rais wa Marekani Joe Biden, ambaye alielezea kuwa Urusi itajibiwa kwa uvamizi mdogo utakaofanywa ndani ya nchi yake.

Rais Biden alikuwa amependekeza kwamba uvamizi mdogo utakaofanywa huenda ukajibiwa kwa kiwango kama hicho kutoka kwa Marekani na washirika wake.

Hata hivyo, Zelensky alituma ujumbe wa twitter akisema: hakuna uvamizi mdogo, sawasawa na kuwa hakuna majeruhi mdogo na huzuni ndogo kutokana na kupoteza wapendwa. Urusi imewaweka wanajeshi 100,000 karibu na mpaka na Ukraine, lakini inakanusha kupanga uvamizi.

Rais Vladmir Putin alitoa masharti , akisisitiza kuwa Ukraine haipaswi kamwe kuruhusiwa kujiunga na Nato na kwamba muungano huo wa kujihami unapaswa kuacha shughuli za kijeshi mashariki mwa Ulaya. Rais Biden aliuambia mkutano wa wanahabari kwamba kiongozi mwenzake Putin angelipa gharama kubwa' kwa kuivamia Ukraine, lakini pia akadokeza kwamba huenda ikategemea jinsi Urusi itakavyotekeleza uvamizi huo.

"Unachokiona ni kwamba Urusi itawajibishwa ikiwa itavamia na inategemea na inafanya nini," alisema.

Maoni yake hayo yaliibua maswali juu ya jinsi Marekani inaweza kujibu uvamizi wa Urusi, na maofisa wamekuwa wakijaribu kufafanua msimamo huo.

"Tumekuwa wazi sana kote," alisema Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken.

Alhamisi ya wiki hii,Biden mwenyewe alisema kwamba kuingia kwa wanajeshi wa Urusi kutachukuliwa kama uvamizi. **BBC**



Moshi ukitanda eneo la migodi baada ya kutokea mlipuko na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 17 katika kijiji cha Bugoso nchini Ghana jana. **(PICHA: BBC)**

# Mlipuko mkubwa waua 17 Ghana

**ACCRA,** GHANA

JUMLA ya watu 17 wanahofiwa kufariki katika mlipuko mkubwa uliotokea karibu na mji mmoja wa migodi mashariki mwa Ghana.

Hata hivyo, idadi hiyo inaweza kuongezeka baada ya kuwepo na hofu kuwa idadi kubwa ya watu wamekufa katika tukio hilo.

Taarifa ya polisi ilisema mlipuko huo ulisababishwa na gari lilokuwa likibeba vilipuzi vya migodi lililogongana na pikipiki karibu na mji wa Bogoso.

Picha zilizosambaa katika vyombo vya Habari zilionyesha moshi mkubwa uliokuwa ukifuka juu ya nyumba zilizoharibiwa na vifusi vilivyotapakaa kila mahali huku wakazi wakiomba msaada.

Katika tukio hilo watu 59 waliripotiwa kuwa walijeruhiwa , baadhi yao wakiwa katika hali mbaya , kulingana na Waziri wa Habari Kojo Oppong Nkrumah.

Rais wa Ghana Nana Akufo Ado, alisema jeshi limekwenda kufanya kazi ya uokoaji ili kusaidia kudhibiti hali ya usalama na kutoa msaada wa dharura kwa raia.

"Ni tukio la kusikitisha, ambalo halikutarajiwa kwa kweli," alisema Rais Ado kupitia ukurasa wake wa Twitter.

Katika taarifa ya dharura, polisi walisema mlipuko huo ulitokea kati ya Bogoso na kijiji cha Bawdie.

Juhudi za uokoaji zilikuwa zikiendelea na watu wametakiwa kuhama eneo hilo.

Polisi walitoa wito kwa miji ya karibu kufungua madarasa yao na makanisa ili kuwahudumia waathiriwa walionusurika.

Kundi la polisi na wataalamu wa milipuko wa jeshi walitumwa kwenda kuzia uwezekano wa mlipuko wa pili na kuimarisha usalama katika eneo la tukio.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

NAFASI ZA KAZI YA UKAGUZI, WA ELIMU SIFA AWE NI MKAGUZI WA ELIMU MSTAAFU 0783 298 900

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **GOOD NEIGHBOURS TANZANIA**, **Sepco Debt Collection & Auctioneering Co, Ltd** tutauza kwa mnada wa hadhara Magari yaliyoko kwenye jeduali,mnada utafanyika katika yard yetu iliyopo tabata kimanga kuanzia saa nne asubuhi,

| Aina ya Gari | Namba ya usaji wa gari | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|
| **Toyota land Cruiser** | T 988 DAE | 28/01/2022 |
| **KIA** | T 263 DEV | 28/01/2022 |
| **KIA** | T 509 CFH | 28/01/2022 |

**MASHART YA MNADA**

Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 7 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi,Gari inauzwa kama ilivyo

**Mawasiliano piga: -**
**SEPCO - 0715-683777/0782-548337**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JOEL JOSEPH MILANZI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina **JACKQULINE JACOB MWAKINGILI** aina ya **TOYOTA PORTE** namba za usajili **T 180 CXB** Chassis No. **NNP110021925,** Engine No.**1NZEAA1925.** Yeyoe atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/27912/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**

**Kituo cha Njombe Mjini Mkoa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 9/2022**

**Katika Shauri la Mirathi ya AHMED RAMADHANI MWASUMILWE………….MAREHEMU**
**Wa RAMADHANI - NJOMBE**

**Katika shauri la maombi ya kumteua Msimamizi yaliyoletwa na FARIDA AHMED MWASUMILWE………………Mwombaji**

**TANGAZO KWA UMMA**

**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 Mwezi wa 01 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu. Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 20 Mwezi wa 01 Mwaka 2022.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KILOSA**
**WILAYA YA KILOSA**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 13 YA 2021**

**MDAI: SALIMA MOHAMED MATEWELE**

**DHIDI YA**

**MDAIWA 1: RASHID ADAM MTOPA**

**MDAIWA 2: ASHA RASHID MTOPA**

**YAH; KUITWA SHAURINI POPOTE PALE ULIPO**

Fahamu kwamba mdai ameleta madai yake dhidi yanu. Madai hayo yamepangwa kusikilizwa Tarehe 08/02/2022. Fahamu kwamba unatakiwa kuhudhulia Mahakamani nyie wenyewe/Wakili wenu siku hiyo bila kukosa. Kutokuhudhuria kwako kutaifanya mahakama hii iendelee na shauri hili bila kuwepo na kulitolea maamuzi. Imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 18 mwezi 01 mwaka 2022

HAKIMU MFAWIDHI WA MAHAKAMA YA WILAYA
KILOSA

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 12 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late ANUSIATH PIUS KIBENA**

**By 1. CASIUS DAMAS PAULO**
**2. ……………………………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 08th day of FEB….. 2022
Dated at MOROGORO this 21st day of JAN………2022

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 11 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late IBRAHIM GURENI MKANZA**

**By 1. TINIHAIKA ABRAHAM MNZAVA**
**2. ……………………………………………….**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above –named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 09th day of FEB….. 2022
Dated at MOROGORO this 21 day of JAN………2022

RESIDENT MAGISTRATE

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-10

**Na Adam Fungamwangwo**
**(0716 350534)**

Jan aliona ni kweli kama Diana angemficha na bila kusema lolote lile, ikiwemo kumtambulisha kwa Chala kama mjomba wake, na siku hiyo Jan ilibidi awe mpole, asingeweza kumpata leo hii.

Wakati Chala alijua kuwa yupo na mjomba wa mpenzi wake aliyemfuata ofisini mwake, Jan alitambua kuwa anayezungumza ni mume mwenzake. Lakini hapo alikuwa anajifanya mjomba wa Diana alivyowahi kumtambulisha kwake.

"Hapana, hizo pesa zinaweza kufilisi kampuni yangu, kwa sababu inaingia shoti na itachukua muda kulilipa mjomba."

"Kwa hiyo wewe una shilingi ngapi ili tukamkomboe Diana."

"Nitatoa shilingi milioni kumi na tano tu."

"Poa lete tu hizo hizo, lakini mpenzi wako akijua kama umetoa kiasi hicho cha pesa, sijui kama mtaelewana tena."

"Unasikia mjomba, mimi nimetoa kiasi hicho, Diana naye ana ndugu zake ambao ndiyo nyinyi, wote inabidi tushirikiane kwa michango ili tufanikishe suala hili." Chala alijibu.

"Haya, zinatakiwa pesa keshi hapa, jamaa hawataki kuwekewa kwenye akauti kwa kuhofu watajulikana na kukamatwa."

"Sawa mjomba."

********************************

"Hallo, hizo pesa zinatakiwa ziwekwe kesho chini ya daraja la Mfugale pale Tazara majira ya saa nane usiku. Kumbuka hatuhitaji ujanja wowote ule. Tukigundua kuwa askari polisi wanaijua hii inshu, basi mtu vipande vya mwili wa mtu wenu vitakwenda kutupwa baharini viliwe na samaki." Ni maneno yaliyotoka kwa mtu aliyepiga simu. Ni mmoja ya watu wanaomshikilia Diana, lakini safari hii hawakutumia simu ile waliyopiga jana.

"Sawa nimekuelewa."

Kengele ya mlango ililia. Baada ya kufunguliwa aliingia mtu anayemfahamu, Jan, lakini akiwa ameongozana na watu wawili. Mmoja alionekana ni mtu mwenye wadhifa, lakini mwingine alikuwa amevaa sare za Jeshi la Polisi.

Hiyo ilimshtua Ken. Alianza kumlaumu kimoyomoyo kwa alichokifanya kijana Jan.

Alichodhani ni kwamba wale wote ni maafisa wa polisi na kwamba tayari Jan suala hilo ameshalifikisha kwenye mkono wa sheria, kitu ambacho watekaji walionya lisifanyike.

"Huyu ni kaka yangu. Ndiyo tuko kwenye pilika pilika ya kukusanya milioni hamsini kwa ajili ya kukomboa Diana."

"Okay, vizuri, shikamoo."Alisalimia. Alikuwa ni Chala ambaye aliletwa hapo na Jan kwa ajili ya kutoa hizo pesa.

"Kaka huyu anaitwa Chala, ni mmoja wa mabosi anakofanyia kazi Diana. Ni yeye tu ndiye anayejua hii habari kuwa jamaa wanataka pesa. Na nimefanya hivi mimi ili kufanikisha jambo hili. Peke yetu kaka tusingeweza."

Ken alitulia tuli. Pamoja na kuona kama vile kijana Jan anafanya vitu sivyo, lakini alimsfu kimoyomoyo kwa jitihada zake kubwa kuhakikisha Diana anaachiwa. Hata hivyo alishangaa kuitwa kaka badala ya mjomba kama anavyoitwa siku zote.

Hakujua kuwa Jan anajuliana kwa Chala kama ni mjomba wa Diana, hivyo yeye mjomba kwa kweli ni lazima awe mdogo au kaka mtu.

"Ana milioni 10 na hizo hapo kwenye mkoba wake."

"Lakini zinazotakiwa ni shilingi milioni hamsini."

"Kaka wewe ongezea ulizonazo, halafu mengine niachieni mimi."

"Mimi kama nilivyosema awali nilichonacho ni shilingi milioni tano."

"Weka, halafu mimi ndiyo nitakwenda kuwapelekea."

Chala na Ken walibaki wakimuangalia Jan kwa mshangao.

Alionekana ni kama anapanga mikakati ya sherehe hivi na si jambo la hatari la kukusanya pesa na kuwapelekea majambazi ambao wamemteka na kumshikilia mtu.

Chala alimkabidhi Ken pesa hizo na baada ya muda akaaga kuwa ana kikao chake yeye na wafanyakazi wake.

Ndani wakabaki Ken na Jan. "Naona ulikuwa unaniita kaka alipokuwa yule mgeni kwa sababu gani?"

"Nilimdanganya kuwa wewe ni kaka yangu, si unajua jinsi unapokwenda kuomba pesa ni lazima uutaje undugu wa karibu."

"Duh, sikujua kama wewe ni mjanja kiasi hiki, ulipajuaje kazini kwa Diana?"

"Alishawahi kunielekeza na kunitajia kampuni yenyewe, ndiyo maana wala sikupata tabu kwenda, nikamtafuta bosi wao, nikaongea naye kirefu na kumpa siri kuwa kinachotakiwa ni pesa ili aachiwe na yeye mfukoni akatoa pesa hizo. Asingeweza kutoa pesa zaidi kwa sababu ingesababisha wafanyakazi wengine kujua na ikisambaa kuwa jamaa wanahitaji pesa wakati wamesema iwe siri itakuwa ni hatari kwa Diana."

Kitu ambacho Ken hakukijua ni kwamba wale wote wawili ni wapenzi wa mpwaye Diana, ila mmoja ameamua kujifanya ni mjomba mtu. Na wakati wanakuja pale, Jan alimwambia Chala kuwa ajifanye ni bosi wa Diana na si mpenzi wake. Kujishusha kama alivyoambiwa na Diana, ndiko kulikomfanya leo kuweza kufanya mbinu hizo za kusaka pesa.

"Kumbuka kuwa leo usiku hizo pesa ndiyo zinatakiwa zipelekwe chini ya daraja la Mfugale, kwa hiyo nakuomba ulale hapa leo. Huwezi kutoka hapa ukaenda nyumbani kwako na kiasi cha pesa kama hiki ni hatari sana."

"Ni kweli mjomba, itabidi leo nilale hapa hapa. Ila saa hizi kuna sehemu tena nakwenda, nikakamilishe vitu fulani kwa kazi hii hii, halafu nitarejea kama saa moja usiku hivi mjomba." Aliaga.




**"Kumbuka kuwa leo usiku hizo pesa ndiyo zinatakiwa zipelekwe chini ya daraja la Mfugale, kwa hiyo nakuomba ulale hapa leo. Huwezi kutoka hapa ukaenda nyumbani kwako na kiasi cha pesa kama hiki ni hatari sana."**

******************************

"Kama wanataka pesa, basi hiyo ni kazi ya Jeshi la Polisi kufanya kazi yake. Haiwezekani mimi nikatoa pesa, wakati naweza kumuokoa Diana kwa nguvu ya jeshi." Ilikuwa ni sauti ya Afande Marco akimjibu Jan.

Safari ya Jan ilimpeleka hadi kwenye Kituo cha Polisi Ubungo ambako alikutana na afande huyo na kueleza kuwa watekaji wamepiga simu na wanataka kitita cha shilingi milioni hamsini.

Afande Marco alimkumbuka Jan kwa sababu alishawahi kuonana naye akiwa na Diana. Alitambulishwa kuwa ni mjomba wake. Ni kama ilivyokuwa kwa Chala. Pia Jan alikuwa anajua kuwa afande Marco ni mpenzi wa Diana. Na kila akikumbuka maneno ya Diana kuwa yeye ndiye mshindi kwa sababu ameweza kumtambulisha kwa wote hao wawili, hivyo yeye anawafahamu, lakini yeye hawamfahamu kuwa naye ni mpenzi wake. Pia hao hawafamiani, lakini yeye anawafahamu wote wawili. Mengine aachiwe yeye kwani muda utaongea.

Akakumbuka maneno ya Diana kuwa hawezi kuwaacha hao wote wawili ghafla kwa sababu wana uwezo wa kipesa na kimamlaka, wanaweza kutafuta chanzo na wakikipata kuwa ni yeye, basi maisha yake yanaweza kuwa hatarini. Mwanya huo ndiyo sasa anautumia Jan kwenye sakata la mpenzi wake kutekwa.

"Mpwa wangu ametekwa na wewe umesikia, wanasema tupeleke kiasi cha shilingi milioni kumi kwenye daraja la Mfugale pale Tazara, leo usiku saa nane, lakini jamaa wamesema tusiwaambie polisi, vinginevyo watamuua. Usingekuwa mpenzi wake nisingekwambia. Kwa sababu wewe ni polisi, lakini nimelazimika kwa sababu pesa zinatakiwa za kuongezea." Afande Marco alihabarishwa.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# UZINDUZI KILI MARATHON WAFANYIKA RASMI MOSHI

**Na Mwandishi Wetu, MOSHI**

UZINDUZI rasmi wa mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon (2022), umefanyika Mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro jana ikiwa ni takribani mwezi mmoja umebakia.

Hafla hiyo iliyowakutanisha wadau mbalimbali, iliandaliwa na Hoteli ya Kibo Palace, moja ya wadhamini wenza wa mbio hizo ambazo hufanyika kila mwaka hapa nchini.

Wadhamini katika hafla ya maadhimisho haya ya miaka 20 ni pamoja na Kilimanjaro Premium Lager (Mdhamini Mkuu) Tigo (21km) na Grand Malt (5km).

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kigaigai, aliwapongeza wadhamini na waandaaji wa mashindano hayo kwa kuhakikisha mbio hizo muhimu katika kukuza sekta ya michezo na uchumi zimeendelea kuwa kivutio kwa wadau wengi wa michezo kwa miaka 20 sasa.

"Hili ni tukio kubwa ambalo linaunufaisha Mkoa wa Kilimanjaro, mikoa ya jirani na taifa kwa ujumla kwa sababu kuna fedha nyingi za kigeni zinazopatikana kutokana na shughuli wanazofanya wageni wanaokuja nchini kabla na baada ya mbio za marathon kufanyika", alisema Kagaigai.

Aliongeza serikali ya mkoa itaendelea kushirikiana kwa karibu na waandaaji na wadhamini wa mbio hizo ili kuhakikisha tukio hilo linaendelea kukua na lengo kuu likiwa ni kuboresha utalii kupitia michezo hapa nchini.

Kiongozi huyo alitoa wito kwa wadau wengine wa michezo kuiga kazi nzuri zinazofanywa na wandaaji wa mbio za Kilimanjaro Marathon.

"Tunawashukuru kwa jinsi mlivyojipanga sana kwani hii inatupa wakati rahisi kama serikali kutoa ushirikiano wetu kutokana na ukweli kuwa mmejipanga vyema huku mkiishirikisha Serikali ya Mkoa, hili linatuweka katika nafasi nzuri na rahisi zaidi katika kuhakikisha kuna usalama wa uhakika kabla na baada ya mbio za Kilimanjaro Marathon," Kigaigai alisema.

Naye Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Irene Mutiganzi, ambaye pia ni Meneja wa Chapa ya Grand Malt, alisema maadhimisho ya 20 ya mbio za Kilimanjaro marathon ni mafanikio makubwa haswa ikitiliwa maanani kuwa wao ndio wadhamini wakuu wa mbio hizo tangu kuasisiwa kwake.

"Mbali na kuwa mashindano ya kimataifa yaliyojijengea umaarufu mkubwa, sisi kama wadhamini wakuu tumehamasishwa kujitolea zaidi kutokana na mbio hizi kuchangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa sekta ya utalii na utamaduni wa Mtanzania kwa ujumla," alisema Mutiganzi.

Alisema washindi wa kwanza kwa upande wa wanaume na wanawake kwa mbio za kilomita 42 watazawadiwa Sh. milioni nne kila mmoja na kwamba Mtanzania mwanamume au mwanamke atakayeshika nafasi ya kwanza katika mbio atapata zawadi ya ziada ambayo ni Sh. milioni 1.5.

Aidha alitoa wito kwa wanaotarajia kushiriki mbio hizo kuhakikisha wanajiandikisha mapema kupitia mtandao wa www.kilimanjaromarathon.com au kupitia TigoPesa kwa kupiga *149*20# pamoja na mbio nyingine za kilomita tano ili kuepuka kukosa fursa hiyo pale namba zitakapokwisha.

"Sisi tukiwa ni wadhamini wa mbio za kilomita 21, maarufu kama Tigo Kili-Half marathon kwa zaidi ya miaka saba sasa, tunatarajia mbio za mwaka huu zitakuwa ni za kusisimua, tunatarajia washiriki zaidi ya 5,000 kutoka ukanda mzima wa Bara la Afrika watashiriki kutokana na kuongezwa kwa thamani ya zawadi za washindi," Mkurugenzi wa Tigo Kanda ya Kaskazini, Henry Kinabo, alisema.

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zinatarajiwa kufanyika Februari 27, mwaka huu kwenye viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.




Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kigaigai (wa pili kushoto) na Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Irene Mutiganzi (mwenye fulana ya njano), wakikata utepe kuashiria uzinduzi wa mbio za 20 za Kilimanjaro uliofanyika katika viwanja vya Kibo Palace Homes Mjini Moshi. Wengine ni wadau wa mbio hizo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Gofu Waitara yanukia Lugalo

**Na Saada Akida**

KLABU ya Gofu ya Lugalo imeandaa shindano maalumu ya mchezo huo la kuwania taji la Waitara Johnnie Walker Trophy litakalofanyika Januari 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lugalo, Kawe jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Gofu Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema lengo la kuandaa shindano hilo ni kukumbuka juhudi za mwasisi wa klabu hiyo, Jenerali, George Waitara.

Luwongo alisema mashindano hayo yatakuwa ya siku moja na ingawa awali yalipangwa kufanyika Novemba, ambapo kwa mwaka jana hawakufanikiwa kuyaendesha kutokana na sababu zilizokuwa nje ya uwezo wao.

"Mwaka huu tutafanya ifikapo Januari 29, hii ni kuenzi juhudi za mwasisi huyo ambaye alianzisha klabu hii, mashindano haya yatakuwa katika kumbukumbu kwa vizazi vijavyo juu ya nani ni mwasisi wa klabu," alisema Luwongo.

Mwenyekiti huyo aliongeza wamewaalika pia wachezaji kutoka klabu zote za hapa nchini ikiwamo Moshi, Arusha Gymkhana, Mufindi, Morogoro Gymkhana, Sea Cliff (Zanzibar), Kili na TPC.

"Shindano hili ni la siku moja ambalo litatanguliwa na wachezaji wa kulipwa watakaocheza siku ya ijumaa, wachezaji wa ridhaa na wanawake watacheza siku ya Jumamosi," aliongeza mwenyekiti huyo.

# Tembo Warriors kambini Februari

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya mpira wa miguu kwa watu wenye ulemavu (Tembo Warriors), inatarajiwa kuingia kambini mwezi ujao kwa ajili ya kuanza maandalizi kuelekea fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika Oktoba, mwaka huu nchini Uturuki.

Tembo Warriors imepata nafasi ya kushiriki fainali hizo baada ya kufanya vizuri katika michuano ya Afrika (CANAF), iliyofanyika hapa nchini mwaka jana.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Yusuph Singo, alisema amekutana na Kamati ya Utendaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu Wenye Ulemavu ((TAFF), ili kuweka mikakati ya pamoja namna timu hiyo itakavyoandaliwa kuelekea michuano hiyo ya dunia.

Singo alisema mikakati hiyo ni pamoja na kufuata maelekezo ya Rais, Samia Suluhu Hassan, aliyotoa kuhakikisha timu za taifa zinaandaliwa mapema kwa lengo la kufanya vyema katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki.

**"Katika kikao hicho serikali imepokea taarifa kutoka Kamati ya Utendaji ya TAFF na kutolea baadhi ya maelekezo yanayotakiwa kufanyiwa kazi kwa haraka ndani ya wiki moja, wamependekeza mengi ikiwamo mwalimu wa timu hiyo awe na sifa gani, kambi kwa wachezaji pamoja na kuongeza wachezaji wengine, tutazidi kujadiliana zaidi kuelekea mashindano hayo," alisema Singo.**

Naye Rais wa TAFF, Peter Sarungi, alisema tayari wameanza vikao vya serikali ili kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri na timu inaimarika.

"Tumekuwa na vikao na serikali kwa ajili ya kupanga maandalizi yetu kuelekea katika fainali za Kombe la Dunia, tunatarajia kuingia kambini mwezi ujao," alisema Sarungi.

Aliongeza anaamini kuanza mapema kwa maandalizi ya timu hiyo kutasaidia kuwajenga wachezaji wao ili kwenda Uturuki wakiwa wenye viwango vya juu na si kusindikiza mataifa mengine.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE SAFI MADRID

KLABU ya Real Madrid inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 23 kutoka PSG na atajiunga kama mchezaji huru wakati mkataba wake utakapokamilika. **(ESPN)**

### NDOMBELE ANUKIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain iko katika mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Tanguy Ndombele mwenye umri wa miaka 25 kwa mkopo. (**Goal**)

### SEVILLA YAMTAKA MARTIAL

SEVILLA bado inataka kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Anthony Martial mwenye umri wa miaka 26 kwa mkopo. (**Marca**)

### LINGARD APATA BARAKA

MANCHESTER United itamruhusu winga wa Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29 kuondoka kabisa mwezi huu, huku Newcastle United ikiwa na nia ya kumsajili. (**Sky Sports**)

### NEWCASTLE YAMWINDA BAKKER

NEWCASTLE United wamewasilisha ombi la dau la pauni milioni 14.5 kumsajili beki wa kushoto wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Mitchel Bakker mwenye umri wa miaka 21. (**Mail**)

### SPURS YAMTAKA KASSIE

KLABU ya Tottenham Hotspur inafikiria kuwasilisha ombi la kumnunua kiungo wa kati wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Francke Kessie mwenye umri wa miaka 25. (**Telegraph**)

### POGBA BADO HAELEWEKI

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba (28), hajaiambia Manchester United iwapo anataka kubakia katika klabu hiyo zaidi ya mwisho wa msimu huu wakati mkataba wake utakapokamilika. Mchezaji huyo anatakiwa na PSG, Real Madrid na Juventus. **(90 min)**

### DEMBELE ATAJWA UJERUMANI

TIMU mbili za Ujerumani zinawania kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24 kwa mkataba wa mkopo. (**Sport**)

### KALU ANUKIA WATFORD

KOCHA wa Watford, Claudio Ranieri amethibitisha klabu hiyo ipo katika harakati za kumsaini winga wa Bordeaux na Timu ya Taifa ya Nigeria, Samuel Kalu mwenye umri wa miaka 24 kwa dau la pauni milioni tatu. (**Evening Standard**)

### CHRISTENSEN AGOMBEWA

BARCELONA na Bayern Munich zinaongoza katika mbio za kumsaka beki wa Chelsea, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 25. (**Fabrizio Romano**)

### ISAK ATAKIWA BARCA

BARCELONA pia wana mpango wa kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22. (**90min**)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ALGERIA YAVULIWA UBINGWA WA AFCON

## ●●● Ni baada ya kupokea kichapo kutoka kwa Ivory Coast na kushindwa...

**DOUALA,** Cameroon

MABINGWA watetezi Algeria wameondolewa katika michuano ya kuwania ubingwa wa Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022), baada ya kukubali kichapo cha mabao 3 -1 kutoka kwa Ivory Coast, hapo juzi.

Algeria ilijikuta ikiruhusu mabao mawili kabla ya mapumziko baada ya Ibrahim Sangare kupokea pasi safi kutoka kwa Franke Kessie na kulipachika goli wavuni.

Nicolas Pepe anayeichezea Arsenal aliipatia Ivory Coast uongozi wa 3-0 kabla ya nahodha wa Algeria, Riyad Mahrez kupoteza penalti.

**Sofiane Bendebka aliifungia Algeria bao la kufutia machozi dakika za mwisho na kuifanya sasa timu hiyo kuyaaga mashindano hayo ikiwa katika Kundi E baada ya ushindani mkali.**

Kikosi cha Kocha, Djamel Belmadi ni mabingwa wa tatu watetezi kuondoka katika awamu ya kwanza ya mashindano hayo katika fainali tano zilizopita za kuwania kombe hilo.

Kuondoka kwao katika mashindano hayo ni tofauti na timu hiyo ilivyoingia, ikielekea Cameroon ikiwa ina ushindi wa kutofungwa mechi 34 na ilitarajia kuipiku rekodi ya Italia ya ushindi mfululizo wa mechi 37.

Algeria ilitoka suluhu na Sierra Leone kabla ya kufungwa 1-0 na Equatorial Guinea na inaondoka na pointi moja kutoka mechi tatu - lakini angalau ilifanikiwa kufunga bao kupitia mkwaju wa dakika za mwisho wa Bendebka, uliotoa matumaini ya ushindani.


LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 861,

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
WEST HAM
1 | 1.97
X | 3.63
2 | 3.63

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# AFCON KUWAKA MOTO 16 BORA



**YOUNDE, Cameroon**

BINGWA mara saba wa taji la soka kwa Mataifa ya Afrika (AFCON), Misri imefuzu katika hatua ya 16 bora, baada ya kuwafunga Sudan bao 1-0 katika mechi yake ya mwisho ya Kundi D.

Timu nyingine katika kundi hilo, Nigeria imemaliza katika nafasi ya kwanza ikiwa na alama tisa na kufuzu baada ya kuifunga Guinea Bissau 2-0.

Mataifa mengine yaliyofuzu katika hatua ya 16 ni pamoja na wenyeji Cameroon, Burkina Faso, Gabon, Senegal, Cape Verde, Guinea, Morocco na Malawi.

Ratiba ya hatua ya 16 bora ya mashindano iliyotoka jana jioni ipo kama ifuatavyo, huku hatua hiyo ikitarajiwa kuanza kesho.

| | | |
|---|---|---|
| Burkina Faso | vs | Gabon |
| Nigeria | vs | Tunisia |
| Guinea | vs | Gambia |
| Cameroon | vs | Comoros |
| Senegal | vs | Cape Verde |
| Morocco | vs | Malawi |
| Ivory Coast | vs | Misri |
| Mali | vs | Equatorial Guinea |

# Aubameyang: Sina tatizo la moyo

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang, amesema moyo wake uko sawa kabisa baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu, wakati PSG, Juventus na AC Milan wakiulizia upatikanaji wa nyota huyo.

Aubameyang mwenye umri wa miaka 32 alirejea jijini London akitokea katika fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika nchini Cameroon kwa uchunguzi wa kimatibabu baada ya kugundulika kuwa na tatizo la moyo.

Baada ya uchunguzi wa kimatibabu, Aubameyang aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram: "Nilirudi London kufanya uchunguzi wa ziada, na nina furaha sana kusema moyo wangu uko sawa kabisa na ni mzima kabisa."

"Nashukuru sana jumbe zote za siku chache zilizopita na tayari nimerejea."

Bado haijaamuliwa iwapo nahodha huyo wa Gabon atarejea Cameroon kwenye michuani ya Mataifa ya Afrika, wakati nchi yake Gabon ikipangwa kuvaana na Burkina Faso hapo kesho katika hatua ya 16 bora.

Aubameyang bado hajacheza mechi yoyote kwenye michuano hiyo.



# 636,800

# ETHIOPIA YATUA ZANZIBAR TAYARI KUIVAA TANZANITE

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Wanawake wa umri chini ya miaka 20 ya Ethiopia, kimetua nchini jana tayari kwa mechi yao dhidi ya Tanzanite Queens itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar, imefahamika.

Tanzanite Queens itaikaribisha Ethiopia katika mechi ya kwanza ya raundi ya nne ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia za Wanawake (U-20), zitakazochezwa nchini Costa Rica baadaye mwaka huu.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, aliliambia gazeti hili jana tayari Ethiopia wameshafika Zanzibar na jana jioni walitarajiwa kuanza mazoezi kujiandaa na mchezo huo.

Ndimbo alisema maandalizi ya mechi hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), yamekamilika na waamuzi na kamisaa wa mchezo huo ambaye anatoka Uganda, Catherine Adipo walitarajiwa kuwasili nchini.

"Maandalizi yanakwenda vizuri, taratibu zote za mchezo zinaendelea kufanyiwa kazi, timu zote mbili ziko Zanzibar, tunachosubiri ni muda na siku ya mchezo,"alisema Ndimbo.

Wenyeji Tanzanite Queens waliweka kambi visiwani humo tangu wiki iliyopita na tayari wameshacheza mchezo mmoja wa kirafiki dhidi ya Kombaini ya Zanzibar ambapo walishinda mabao 6-0.

Tanzanite Queens ilisonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuwaondoka wenzao wa Eritrea na Burundi.




Mshindi wa SportPesa Jackpot bonus, Elibariki Magaa kutoka Tabora akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 21.7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 katika Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii ni Sh. milioni 861.6. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Magaa autaja mkeka wa usiku

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Masanga, Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Elibariki Magaa (33), ameibuka mshindi wa Jackpot Bonus ya Sportpesa kwa wikiendi iliyoisha baada ya kupatia kwa usahihi ubashiri wake wa mechi 12 kati ya mechi 13.

Magaa ambaye ni msanii wa fani ya kuchora na usanifu aliweka mkeka wake wa Jackpot usiku wa kuamkia Januari 15, mwaka huu na kufanikiwa kushinda kitita cha Sh. milioni 21.7 na kuwa mshindi pekee wa Jackpot Bonus kwa timu 12, kwa wiki iliyoisha.

Akizungumza baada ya utambulisho na makabidhiano ya mfano wa hundi ya malipo yake, Magaa alisema yeye alianza kucheza na Sportpesa miaka mitatu iliyopita.

"Ni maajabu kweli kweli, kwani uwezo wangu wa kushinda mechi ulikuwa ni wastani wa mechi nane hadi tisa, haya ni mafanikio makubwa sana kwangu kwa kuweza kufikisha mechi 12. Nakumbuka siku ya Ijumaa iliyopita, ilipofika mida ya alasiri, nilifungua app ya Sportpesa na kuchagua mechi na kuziacha bila kuweka ubashiri. Lakini ilipofika usiku wa manane niliona ni muda muafaka wa kuweka mkeka wangu kabla sijalala. Kilichofuatia ndio huu ushindi wa Jackpot Bonus ya mechi 12," alisema Magaa.

Naye Meneja Uhusiano wa Kampuni ya Sportpesa, Sabrina Msuya alisema kwa wiki hiii Jackpot imesimamia Sh. milioni 861.6, hivyo amewaasa Watanzania kuendelea kucheza zaidi Jackpot ili na wao wapate fursa ya kushinda kama ambavyo Magaa na wengine walioshinda.

## JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/01/22 | 18:00 | Zaragoza vs Valladolid | 2.94 | 3.08 | 2.41 |
| 02. 22/01/22 | 18:30 | Moreirense vs Santa Clara | 2.41 | 3.15 | 2.91 |
| 03. 22/01/22 | 20:15 | Fuenlabrada vs Las Palmas UD | 2.99 | 3.04 | 2.40 |
| 04. 22/01/22 | 21:00 | Tondela vs FC Vizela | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 05. 22/01/22 | 23:00 | Malaga vs UD Ibiza Eivissa | 2.34 | 3.14 | 2.99 |
| 06. 23/01/22 | 16:00 | Granada vs Osasuna | 2.51 | 3.16 | 2.91 |
| 07. 23/01/22 | 16:00 | Burgos vs Leganes | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 08. 23/01/22 | 16:00 | Giresunspor vs Alanyaspor | 2.63 | 3.18 | 2.63 |
| 09. 23/01/22 | 19:00 | Galatasaray vs Trabzonspor | 2.55 | 3.19 | 2.70 |
| 10. 23/01/22 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.80 | 2.95 | 2.75 |
| 11. 23/01/22 | 22:00 | Waalwick vs Fortuna Sittard | 2.32 | 3.35 | 2.85 |
| 12. 23/01/22 | 22:45 | AC Milan vs Juventus | 2.66 | 3.26 | 2.66 |
| 13. 23/01/22 | 23:00 | Alcorcon vs Mirandes | 2.65 | 3.09 | 2.65 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 22/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 5293 | Everton vs Aston Villa | 2.69 | 3.29 | 2.60 |
| 16:00 | 1774 | Levante vs Cadiz CF | 1.79 | 3.60 | 4.49 |
| 16:00 | 3814 | Mtibwa Sugar vs Simba | 8.26 | 3.84 | 1.39 |
| 16:00 | 3944 | Biashara United vs Geita Gold FC | 2.19 | 2.74 | 3.60 |
| 16:00 | 4257 | Sivasspor vs Fenerbahce | 2.70 | 3.14 | 2.60 |
| 16:00 | 4268 | Adana Demirspor vs Fatih Karagumruk | 1.96 | 3.36 | 3.76 |
| 17:00 | 2479 | Genoa vs Udinese | 3.34 | 3.29 | 2.19 |
| 17:30 | 1695 | Bayer Leverkusen vs Augsburg | 1.43 | 4.77 | 6.36 |
| 17:30 | 3955 | Monchengladbach vs Union Berlin | 2.23 | 3.43 | 3.08 |
| 17:30 | 4616 | Greuther Furth vs Mainz | 4.48 | 3.64 | 1.76 |
| 17:30 | 5037 | Hoffenheim vs Borussia Dortmund | 2.94 | 3.88 | 2.14 |
| 17:30 | 5092 | SC Freiburg vs Stuttgart | 1.94 | 3.48 | 3.83 |
| 18:00 | 1115 | Kelty Hearts FC vs St Johnstone | 5.60 | 4.15 | 1.47 |
| 18:00 | 1320 | Dunfermline vs Inverness | 3.23 | 3.28 | 2.12 |
| 18:00 | 2497 | Plymouth vs Lincoln | 1.93 | 3.48 | 3.63 |
| 18:00 | 2710 | Blackpool vs Millwall | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 18:00 | 2722 | Livingston vs Ross County | 2.17 | 3.23 | 3.04 |
| 18:00 | 2788 | Coventry vs QPR | 2.35 | 3.24 | 2.90 |
| 18:00 | 2830 | Bournemouth vs Hull City | 1.56 | 3.88 | 5.50 |
| 18:00 | 2853 | West Bromwich vs Peterborough | 1.32 | 4.82 | 8.85 |
| 18:00 | 2876 | Manchester Utd vs West Ham | 1.97 | 3.63 | 3.63 |
| 18:00 | 3423 | Leeds vs Newcastle | 1.98 | 3.74 | 3.49 |
| 18:00 | 4105 | Peterhead vs East Kilbride | 1.24 | 5.58 | 8.66 |
| 18:00 | 5013 | Banks O'Dee FC vs Raith Rovers | 10.60 | 6.17 | 1.19 |
| 18:00 | 5024 | Clyde vs Queens Park | 3.09 | 3.33 | 2.17 |
| 18:00 | 5283 | Motherwell vs Morton | 1.45 | 4.03 | 6.15 |
| 18:00 | 5764 | Aberdeen vs Edinburgh City | 1.04 | 9.64 | 27.96 |
| 18:00 | 5852 | Ayr United vs St Mirren | 2.89 | 3.18 | 2.27 |
| 18:15 | 1180 | Villarreal vs Mallorca | 1.40 | 4.61 | 7.62 |
| 18:15 | 1293 | Kortrijk vs Eupen | 1.87 | 3.54 | 3.88 |
| 18:15 | 1984 | OFI Crete vs Panetolikos | 1.91 | 3.45 | 3.80 |
| 18:30 | 5384 | Emmen vs NAC Breda | 1.73 | 3.66 | 4.29 |
| 19:00 | 1811 | Basaksehir vs Goeztepe | 1.93 | 3.31 | 3.95 |
| 19:00 | 4070 | Brest vs Lille | 3.18 | 3.48 | 2.16 |
| 19:00 | 4142 | Ankaragucu vs Denizlispor | 1.34 | 4.62 | 7.32 |
| 20:00 | 1189 | Inter vs Venezia | 1.10 | 9.21 | 23.03 |
| 20:30 | 2346 | Alloa Athletic vs Celtic | 24.03 | 9.61 | 1.05 |
| 20:30 | 3029 | Kfco Wilrijk vs OH Leuven | 3.01 | 3.46 | 2.20 |
| 20:30 | 3066 | VfL Bochum vs FC Koln | 3.09 | 3.44 | 2.22 |
| 20:30 | 3787 | Sevilla FC vs Celta Vigo | 1.76 | 3.56 | 4.71 |
| 20:30 | 4569 | Southampton vs Manchester City | 8.42 | 5.31 | 1.33 |
| 20:50 | 4224 | Maccabi Haifa vs Hapoel Katamon | 1.16 | 5.98 | 14.47 |
| 21:00 | 5965 | Tondela vs FC Vizela | 2.77 | 3.22 | 2.48 |
| 22:00 | 2396 | Heerenveen vs PEC Zwolle | 1.96 | 3.34 | 3.68 |
| 22:00 | 5341 | AZ Alkmaar vs Cambuur | 1.33 | 5.30 | 7.06 |
| 22:45 | 1255 | Lazio vs Atalanta | 3.06 | 3.66 | 2.18 |
| 23:00 | 1965 | Lens vs Marseille | 2.53 | 3.37 | 2.68 |
| 23:00 | 3573 | Atletico Madrid vs Valencia | 1.49 | 4.22 | 6.63 |
| 23:00 | 5286 | Willem II Tilburg vs Twente | 3.14 | 3.19 | 2.23 |
| 23:30 | 4415 | Sporting Lisbon vs Sporting Braga | 1.57 | 3.90 | 5.53 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumamosi Januari 22, 2022

Nipashe

UKURASA 22



Aubameyang: Sina tatizo la moyo



Straika wa Yanga, Heritier Makambo, akifanya mazoezi ya viungo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Polisi Tanzania itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha. **PICHA: MTANDAO**

## Yanga yafunga hesabu

**Na Dennis Fusi**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema kikosi chake kimeshakamilisha maandalizi kuelekea mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Polisi Tanzania itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Nabi alisema mechi ya kesho itakuwa tofauti kwa sababu zinakutana timu ambazo zimebadilisha wachezaji wake kwa asilimia kubwa tofauti na walivyokuwa msimu uliopita.

Kocha huyo alisema anajua wapinzani wao wamejipanga kuendeleza rekodi nzuri dhidi yao lakini wafahamu mpira wa Yanga umebadilika.

Alisema anafahamu mechi zote za ligi ni ngumu na Yanga imejiandaa kukabiliana na ushindani kwa ajili ya kufikia malengo ya kutwaa ubingwa msimu huu.

"Yanga hii ni tofauti, ni timu nyingine, ina wachezaji wapya, tunabadilika kulingana na aina ya mpinzani, nina matarajio utakuwa mecho mzuri lakini si rahisi," alisema Nabi.

Aliongeza wachezaji wote walioko Arusha wako tayari kwa mechi hiyo na anafurahi kuona ushindani wa kuingia kwenye kikosi cha kwanza umeongezeka.

"Tuna kikosi kilichokamilika, kila mmoja ana nafasi ya kuanza, hili ni jambo jema kwa timu na inatusaidia katika kupanga kikosi, tumejiandaa kuendeleza kasi yetu," alisema kocha huyo raia wa Tunisia.

# Simba kuishangaza Mtibwa

●●●Ni aina ya soka watakalocheza ili kuwafuta machungu mashabiki wao...

**Na Waandishi Wetu**

IKIWA imepita miaka 23 haijakanyaga katika ardhi ya Turiani, Mabingwa watetezi, Simba wanatarajiwa kuwakabili wenyeji Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Manungu, mkoani Morogoro.

Simba itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mchezo wake uliopita dhidi ya Mbeya City uliochezwa Jumatatu iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Katika kuhakikisha inakuwa imara, Simba huenda leo ikamchezesha mara ya kwanza kiungo mshambuliaji wake raia wa Zambia, Clatous Chama ambaye amerejea klabuni hapo kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili akitokea RS Berkane ya Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, alisema amekiandaa kikosi chake kucheza mfumo tofauti na ulioonekana katika mechi iliyopita kwa ajili ya kuhakikisha wanamiliki mpira na wanafanya vizuri katika mchezo huo.

Pablo alisema anafahamu mchezo utakuwa mgumu kutokana na ubora wa wapinzani wao lakini benchi lake la ufundi pamoja na wachezaji wamesema wako imara kuhakikisha hawafanyi makosa katika mechi hiyo. "Tumebanwa na ratiba ngumu ndani ya kikosi, lakini tuko tayari na mapambano. Safari siyo tulivu, hasa kwenye viwanja ambavyo si vizuri kucheza soka tunalolitaka, kwa kiasi fulani wiki hii tulikuwa na mazoezi kwa hiyo kesho (leo), tutacheza mpira tofauti na mchezo uliopita," Pablo.

Alisema wamekuwa na mechi ngumu tatu ugenini ndani ya siku 10, lakini pamoja na hayo hakuna namna wameendelea kujipanga kuhakikisha wanarejea kwenye ushindani kwa kuendeleza kasi ya ushindi waliyoanza nao msimu huu.

Aliongeza tayari wamefanyia kazi mapungufu yao yaliyojitikeza katika mchezo uliopita na sasa wako kamili kukutana na Mtibwa Sugar ambayo pia imedhamiria kulinda heshima ikiwa nyumbani kwake.

Alisema baadhi ya wachezaji wake wa kikosi cha kwanza atawakosa katika mchezo huo lakini ana imani kubwa na nyota waliokuwa kwenye mipango yake leo kwa ajili ya kutimiza majukumu yao na kuwapa furaha mashabiki wa Simba.

"Clatous Chama atakuwa miongoni mwa wachezaji walioko katika mipango yangu kuelekea mchezo wa kesho (leo), naamini wote watakaopata nafasi wataonyesha kile tunachokitarajia," Pablo aliongeza.

Naye Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar, Salum Mayanga, aliliambia gazeti hili kikosi chake kipo tayari kuhakikisha wanabakiza pointi tatu muhimu nyumbani.

Mayanga alisema Simba ni wazuri na ana imani mchezo huo utakuwa na ushindani kwa sababu wapinzani wao wametoka kupoteza mechi iliyopita.

"Tumejiandaa vizuri, Simba ni timu kubwa tena mabingwa watetezi wa ligi hii, lakini pia wametoka kufungwa, watakuja tofauti na tulivyowaona wakicheza, tutacheza kwa kuwaheshimu ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Mayanga.

Kocha huyo alisema anahitaji wachezaji wake kuongeza utulivu wanapokuwa na mpira lakini wakicheza kwa tahadhari ili kufikia malengo yao.

"Tunahitaji pointi kama ambavyo wenzetu wanazihitaji, tumejiandaa vizuri na hatuna wasiwasi wowote hasa ukizingatia tunacheza kwenye uwanja wetu ambao tumeuzoea," Mayanga alisema.

Wakati huo huo, mashabiki wa soka wa kwanza 10 watakaohudhuria mechi kati ya Mtibwa na Simba leo na kukubali kupata chanjo ya UVIKO-19 wataingia uwanjani i bure kushuhudia mchezo huo. Msemaji wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema kwa kutambua umuhimu wa chanjo hiyo, wanatoa rai kwa wananchi wakiwamo mashabiki wa mpira wa miguu kupata chanjo hiyo.

Beki wa timu hiyo, Abdi Banda alisema alishapata chanjo hiyo baada ya kujua umuhimu wake na alifanya hivyo ili kujilinda na kuilinda familia yake.

***Imeandaliwa na Adam Fungamwango, Saada Akida na Idda Mushi, Morogoro***

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >